bible educational services

# Mwongozo kwa Waalimu

## Wakati na Biblia Daraja la sifuri, la kwanza na la pili

Mfululizo wa C
Somo la saba hadi kumi na mbili

www.besweb.com

## Bible Educational Services

Registered Charity UK (No 1186004)
Imesajiliwa kama shirika la Hisani Uingereza (Namba 1186004)

**Dhamira**
Kuandaa masomo ya Biblia kwa ajili ya wadau ili kutumika kuwakilisha kweli ya Yesu Kristo kwa kizazi kijacho ulimwenguni kote.

**Maono**
Kufikia kizazi kijacho kwa lugha zao kwa kutumia mtaala wetu kamili kwa kukuza na kusaidia mtandao wa kimataifa wa wabia wanaojitolea.

## HABARI KWA UJUMLA

**Bible Educational Services hufanya nini:**

Bible Educational Services (BES) huchapisha masomo ya Biblia ya "Wakati na Biblia/Bibletime", "Maisha Mapya/New Life" na "Wakusanyaji/Gleaners" kwa Lugha ya Kiingereza na kusaidia vituo vya Shule ya Biblia kwa njia ya Posta pamoja na mashirika mengine ya namna hiyo yanayotumia masomo ya BES huko Uingereza na nchi zingine. BES hufanya hivi kwa kutembelea, kutoa ushauri, kutoa mafunzo na kuunganisha mashirika haya na mengine. Sasa hivi, BES inafanya kazi na vikundi mbalimbali kutoka nchi zingine, vinavyohusika na kutafsiri, kubuni, kuchapisha na kusambaza masomo. Masomo haya yanatolewa bure kabisa kwa kila mtoto.

Kwa mara ya kwanza, masomo ya Wakati na Biblia yalitumika huko Kusini mwa Ireland (Uingereza) zaidi ya miaka sitini iliyopita. Bible Educational Services (BES) wameendelea kuchukua jukumu la uhariri wa masomo ya Wakati na Biblia kwa lugha ya Kiingereza na Lugha zingine. Kwa muda mrefu, Masomo ya Wakati na Biblia (Bibletime) yalichapishwa kwenye muundo wa A4 ambao uliwawezesha wanafunzi kutoka baadhi ya maeneo kutuma masomo yao kwenye kituo cha BES kwa ajili ya kusahihishwa kila baada ya wiki nne. Hivi karibuni, masomo ya miezi sita yamechapishwa kwa muundo wa A5. Muundo huu umefanya utumiaji wa masomo haya uwe rahisi na wa kufaa zaidi kwa makanisa na shule ambazo hazina ufanisi mzuri wa mfumo wa njia ya posta. Tunawashukuru Every Home Crusade au Revival Movement huko Belfast Uingereza kwa kutuwezesha kufanya hivi.

Masomo ya BES ni ya kipekee kwa sababu yameandaliwa ili kutumika nyumbani au kwenye vikundi kama vile kutoka kwenye makanisani na kwenye shule. Masomo haya yameandaliwa kwa kuzingatia vyema mtaala (Syllabus). Masomo yamepangiliwa vizuri na unaomruhusu mwanafunzi kuyatumia hadi atakapotimiza umri wa miaka 20. Masomo yanapatikana katika madaraja matano ambayo yamezingatia umri tofauti. Nayo ni, masomo kwa ajili ya watoto wa chekechea (Daraja 0) ambao wana umri wa chini ya miaka mitano, miaka mitano hadi saba (Daraja la 1), miaka nane hadi kumi (Daraja la Pili), miaka kumi na moja hadi kumi na mitatu (Daraja la Tatu) na miaka kumi na minne hadi kumi na sita (Daraja la Nne). Kuna Mtaala wa miaka mitatu katika kila kikundi cha umri (angalia ukurasa wa 4). Vikundi hivi vya umri vinaweza kutofautiana kulingana na uwezo tofauti wa watoto. Rasilimali na masomo ya Wakati na Biblia yanawapa watoto fursa ya kujifunza Neno la Mungu, kujifunza Habari za Biblia na kujifunza kukabiliana na changamoto zinazotokea maishani mwao kulingana na mwongozo wa Injili ya Bwana Yesu Kristo.

Nakala zilizochapishwa za masomo kwa Lugha ya Kiingereza zinapatikana kwenye tovuti ya BES /BES website – www.besweb.com au kwa katibu ofisi ya BES Uingereza. Yanapatikana pia kwa lugha zingine kwenye tovuti. Kwenye tovuti kuna nyaraka muhimu kwaajili ya mtu yeyote au shirika linalopenda kushirikiana nasi.

## Anuani za mawasiliano za BES

**Ofisi ya Uingereza (Northern Ireland) (Mhifadhi wa masomo yote ya Kiingereza)**
37a Belmore Street, Enniskillen, Northern Ireland BT74 6AA
Simu: +44 286 632 2462

**Katibu wa Uingereza**
Bw. Stephen Gillham,
Barua pepe: stephen.gillham@besweb.com

Tovuti: www.besweb.com
Barua pepe: info@besweb.com

**Mshirika Tanzania (Tanzania Partner)**
World Vision Tanzania
S.L.P. 6070 Arusha, Tanzania
Barua Pepe ya Mawasiliano: david_ombeni@wvi.org
Simu: +255 687 231 757

## MWONGOZO kwa WAALIMU

Mwanzoni, masomo ya Wakati na Biblia yaliandaliwa ili yatumike kwa njia ya posta kukiwepo na kituo cha Shule ya Biblia kwa njia ya posta. Sasa hivi, masomo yanaendelea kutumika kwa wingi hata kwenye sehemu ambazo hazina ufanisi wa kutumia mfumo wa posta au hakuna kabisa mfumo wa posta hasa katika makanisa na shule zilizopo Afrika, India na maeneo mengine. Mwongozo kwa Walimu umeandaliwa kwa wale wanaotumia masomo ya Wakati na Biblia katika hali kama hizo. Mwongozo kwa Walimu katika kitabu hiki umeandaliwa kutumika kwa masomo ya Daraja 0, Daraja la kwanza na Daraja la pili kwa watoto wenye umri kutoka chekechea hadi wastani miaka 10. Masomo ya Daraja 0 hayajajapishwa ila yanaweza kupakuliwa bure kwenye tovuti ya BES.

Kila Mwongozo wa kufundisha hufuata vifungu vile vile vya Biblia vilivyopo katika somo la Wakati na Biblia. Masomo ya Wakati na Biblia na Mwongozo vimeandaliwa vitumike kila wiki. Masomo ya mwezi Aprili yanahusu Pasaka na masomo ya mwezi Desemba yanahusu Krismasi.

Baadhi ya sehemu watakuwa wanatumia masomo yaliyo katika toleo la A4 la kila wiki na wengine watakuwa wanatumia kitabu cha A5 chenye masomo 24 ndani yake. Kwa kawaida, mwalimu au kiongozi hutoa somo la mwezi toleo la A4 na kila wiki sehemu ya kazi hujazwa kanisani au shuleni au hupelekwa nyumbani na kurejeshwa wiki inayofuatia. Mwishoni mwa mwezi, mwalimu au kiongozi hukusanya somo na kwenda kusahihisha kama inavyotakiwa na kumrudishia mwanafunzi/mtoto kazi iliyosahihishwa mapema iwezekanavyo.

Unapotumia kitabu, mwisho wa kila kipindi, vitabu hukusanywa na kusahihishwa. Tumegundua katika sehemu nyingi kuwa, hili haliwezekani. Hivyo basi, pale darasani masomo yanaweza kugawanywa kwa wanafunzi wengine na mwalimu au kiongozi ataongoza usahihishaji wa somo na wanafunzi watasahihisha masomo ya rafiki zao na kutoa maksi. Nyuma ya kitabu kuna sehemu kwa ajili ya kuweka maksi ya kila somo la mwezi na pia mahali pa maoni kuhusu maendeleo ya mwanafunzi. Pia kuna cheti ambacho mwanafunzi anaweza kupewa kinachoonesha asilimia ya alama ambazo mwanafunzi amepata kwa masomo ya miezi sita.

## MAANDALIZI KWA WAALIMU

Mwongozo huu wa Walimu siyu shinikizo ambao hauwapi walimu fursa ya kufanya mambo kwa njia zao wenyewe kulingana na mawazo na mipango yao wenyewe. Haya ni mapendekezo yanayoweza kutumika kwenye utumiaji wa masomo ya Wakati na Biblia.

- **Elewa habari vizuri** – Walimu wanapaswa kuelewa habari ya Biblia vizuri kwa kadiri iwezekanavyo na vile vile somo la Wakati na Biblia linaloendana na habari hiyo ya Biblia. Ni jambo zuri kwa mwalimu kukamilisha somo la Wakati na Biblia kabla ya kipindi. Mwongozo wa kila somo unapaswa kutumiwa kwa umakini kama chombo cha kumsaidia mwalimu anapojiandaa kwa ajili ya somo.
- **Elewa funzo ambalo watoto wanastahili kupata au kujifunza** – Juu ya kila mpangilio wa somo utaona maneno ‘Tunajifunza kuwa’ ikifuatiwa na makusudio mawili ya kujifunza ambayo tunatumaini kwamba watoto watayaelewa baada ya kumsikiliza mwalimu akifundisha na kukamilisha somo la Wakati na Biblia. Kusudio la kwanza la kujifunza jambo linahusu ufahamu wa habari na la pili linamtia moyo mtoto kufikiri juu ya ufahamu huo, kuutumia na kuuitikia. Makusudio haya ya kujifunza ni sentensi kamilifu na fupi ya mawazo au kweli kuu zinazofundishwa katika somo. Walimu wanaweza kuzitumia kwa ajili ya tathimini zao binafsi za ufundishaji na mafunzo ambayo watoto wamepata.
- **Toa Utangulizi** – Kwa masomo yote, tunaanzia mahali ambapo watoto wapo katika uzoefu wao wa hali husika. Tumependekeza njia kadhaa ambazo zinaweza kutumika kufanya utangulizi wa habari ili kuwawezesha watoto kuhusika katika kujadili mwanzo wa habari.
- **Fundisha** – Tumetoa dondoo muhimu katika habari. Tunaamini kwamba walimu hawatazinukuu wakati wanafundisha habari lakini watakuwa na uelewa mzuri wa habari na wataweza kuifundisha katika njia inayofurahisha na kusisimua. Mwalimu atahitaji watoto waelewe mafunzo muhimu kutoka kwenye habari na kuwasaidia kuuelewa mwitikio watakaoupata kutoka kwenye habari waliyojifunza. Kwa usahihi, tumejaribu kuweka pamoja baadhi ya maelezo kwa ajili ya kufundisha habari. Haya yameandikwa katika maandishi *YA MCHALAZO (Italics)*.
- **Jifunze** – Kuna Mstari Muhimu ambao umewekwa katika kila habari. Katika baadhi ya maeneo, kuna Mistari Muhimu miwili. Mstari huu ulioongezwa unaweza kuwa rahisi kwa watoto kujifunza. Tunatumaini kwamba, watoto watajifunza Mistari muhimu na watakumbushiwa mstari huo mara nyingi iwezekanavyo ili waanze kujenga ufahamu wa Mistari muhimu ya Biblia.

- **Kamilisha** – Katika mazingira ya shule, utatambua uwezo wa watoto kwenye kukamilisha kazi na kiasi cha usaidizi ambao wanauhitaji kutoka kwa mwalimu. Kwa baadhi yao, itahitajika mwalimu asome maandishi katika somo na watoto kufuatilia habari ambayo sasa watakuwa wanaielewa. Watoto wengine wanaweza kusoma maandishi ya somo peke yao. Kwa hali yoyote kati ya zilizotajwa, ni wazo zuri kuwahamasisha watoto wawe makini na kuwapa maelekezo muhimu yanayohusiana na maswali. Kama unatumia masomo ya Wakati na Biblia katika maeneo ambayo siyo shule, ni muhimu walimu kuwepo na kuwasaidia watoto ili wasichukulie masomo haya kama kazi isiyo na mvuto au kama mtihani. Masomo haya yanapaswa kuwa ya kufurahisha na kutia moyo. Ni muhimu kuwasifia watoto wanapoendelea kufanya masomo na kujibu maswali.
- **Kumbuka** – Tunashauri matumizi ya maswali mafupi na maigizo ili kuwasaidia watoto kujifunza na kurudia habari ili kuielewa vyema.
- **Kuonesha** – Tunatambua kuwa katika baadhi ya mazingira, sio rahisi kupata vielelezo au video. Lakini, ni muhimu kadiri iwezekanavyo kuwa na picha au vitu vinavyoweza kuwasaidia watoto kuielewa habari vizuri zaidi. Vielelezo vitakuwa muhimu sana wakati ambapo mwalimu anaelezea habari. Kadiri iwezekanavyo kwenye kila somo, tumetoa maelezo kuhusu picha kutoka kwa picha za www.freebibleimages.org (FBI) ambazo zinaweza kupakuliwa bure kwenye tovuti yao. Mwisho wa Mwongozo wa Walimu kuna viambatisho vyenye viungo (hyperlinks) vya picha tofauti na zinazofaa kwa kila habari kutoka kwenye tovuti ya Free Bible Images. Kama kuna kinakilishi (photocopier), baadhi ya picha za Bibletime zinaweza kufanywa kuwa kubwa, kupakwa rangi na kutumiwa kufundisha.

## Kupangilia Muda

- **Ratiba –** Tumeweka ratiba sawa kwenye mwongozo wa kufundisha kila somo lakini mwalimu anaruhusiwa kubadilisha ratiba hii mara kwa mara kulingana na mahitaji ya darasa lake/ watoto anaowafundisha.
    1. Utangulizi na kuwaambia watoto habari husika – Takriban dakika 15
    2. Kufundisha Mstari muhimu – dakika 5 hadi10
    3. Kujaza nakala ya somo – dakika 20
    4. Maswali na shughuli zinginezo- dakika 5 hadi10

Kumbuka msemo muhimu:

“Niambie na nitasahau,
Nioneshe na nitakumbuka,
Nihusishe na nitaelewa”

## Mtaala wa Wakati na Biblia

| | Daraja 0 (Chekechea/Chini ya miaka mitano) Daraja la Kwanza (Miaka mitano hadi saba) Daraja la Pili (Miaka nane hadi kumi) | Daraja la Tatu (Miaka kumi na mmoja hadi kumi na mitatu) | Daraja la Nne (Miaka kumi na minne na zaidi) |
|---|---|---|---|
| SOMO LA KUANZIA | Somo la kuanzia – Utangulizi (Inaandaliwa) | Somo la kuanzia – Utangulizi (Inaandaliwa) | Somo la kuanzia – Utangulizi (Inaandaliwa) |
| MFULULIZO WA A | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Ibrahimu<br>6. Ibrahimu<br>7. Petro<br>8. Petro<br>9. Yakobo<br>10. Wakristo wa Kwanza<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maombi<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo na Kuanguka<br>2. Matukio ya Kwanza-Mwanzo<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maisha ya Ukristo<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi |
| MFULULIZO WA B | 1. Maisha ya kwanza ya Kristo<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Mifano<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Walioandika vitabu vya Injili<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yakobo na familia yake<br>7. Yusufu<br>8. Matendo ya Mitume 2: 42 – Njia iliyoko mbele<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Amri<br>12. Habari ya Krismasi |
| MFULULIZO WA C | 1. Danieli<br>2. Miujiza zaidi<br>3. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu na Samweli<br>6. Daudi<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Yona<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>3. Miujiza zaidi<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8 Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu ambao Mungu aliwatumia – Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Maneno ya Kristo<br>3. Nguvu za Bwana<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu zaidi wa Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi |

<u>**C7 Habari ya Kwanza**</u>

**Daudi akimbia asiuawe – Habari hii inahusu rafiki mkubwa wa Daudi.**

**Tunajifunza kuwa:**
- Yonathani alidhihirisha kuwa alikuwa rafiki mzuri kwa jinsi alivyomsaidia Daudi.
- Bwana Yesu anaweza kuwa Rafiki yetu.

**Mstari Muhimu:** ***1 Samweli 20:17***
**Habari kwenye Biblia:** ***1 Samweli 20:1-42***

**TOA UTANGULIZI**

Watoto wa Daraja la pili wanaweza kutumia dakika moja au mbili na marafiki wakifikiria kuhusu sifa zinazofanya mtu awe rafiki mzuri. Kisha wanaweza kushirikisha majibu yao katika kundi zima. Ikiwezekana yaandike majibu yao kwa kifupi ubaoni. Sisitiza sifa ambazo rafiki anaweza kuonyesha kama mtu anapitia wakati mgumu k.m. rafiki kusaidia, kulinda, na wakati wote kupatikana. Jaribu kutoa mifano ya hali halisi ambazo zinafaa kwa kundi hilo.
Vinginevyo, kwa watoto wa Daraja la kwanza, unaweza kuwa na mfuko wa vitu vinavyosaidia ulinzi k.m. kofia ngumu (helmeti), krimu ya kujipaka wakati wa joto, dawa ya meno na brashi, glavu ya joto, picha ya mkanda wa usalama, n.k. Chagua mtu mmoja achague kitu kimoja na kusema jinsi kinavyomlinda. Eleza kuwa Mungu anatupa watu wa kusaidia tuwe salama - wazazi, watu wazima wengine (wataje), marafiki. Katika habari ya leo, tutajifunza jinsi rafiki mkubwa wa Daudi alivyomlinda.

**FUNDISHA**

- *Rejelea maisha ya Daudi kama yalivyoshughulikiwa katika C6 kwa kuuliza maswali muhimu: Mpango wa Mungu kwa ajili ya maisha ya Daudi ulikuwa upi? Nani alikuwa mfalme wakati Daudi alipoambiwa angekuwa mfalme ajaye? Waambie watoto kuwa Sauli alimuonea wivu Daudi. Waambie wajiulize ni kwa nini. Sababu zinaweza kuwa ni pamoja na kumuua Goliathi, kushinda vita zaidi, kuwa na Mungu upande wake. Wakumbushe watoto jinsi wivu wa Sauli ulivyojidhihirisha (C6 habari ya 4). (Kwa Daraja la pili, unaweza kuchunguza jinsi wivu unavyoweza kuathiri watoto na kile ambacho Biblia inasema kuhusu wivu)*
- *Wakumbushe watoto kuhusu mwana wa Sauli, Yonathani ambaye alikuwa rafiki mkubwa wa Daudi. Rejelea sifa zinazomuelezea Yonathani kwenye orodha yako iliyotengenezwa kwenye "Toa utangulizi".*
- *Mfalme Sauli alifanya karamu kubwa iliyodumu kwa siku kadhaa. Daudi alitarajiwa kuhudhuria lakini aliona kuwa ilikuwa salama zaidi kutohudhuria. Yonathani alikuwa tayari kumsaidia Daudi na kuchunguza kama Sauli alikuwa akipanga kumdhuru. Alipanga kukutana kwa siri na Daudi shambani baadaye. Huko, angetumia ishara kumwonyesha Daudi kama yuko salama au hatarini.* ***(1 Samweli 20:4-23)*** *Elezea kuwa Mungu alikuwa akimtunza Daudi kwa kumpa rafiki wa pekee wa kumlinda.*
- *Sauli aligundua kuwa Daudi hayupo katika siku ya pili ya karamu. Elezea mwitikio wake.* ***(1 Samweli 20:27-34)*** *Unadhani Yonathani alijisikiaje? Tabiri Yonathani atafanya nini baadaye. Je, atakuwa mwaminifu kwa Daudi na kumwambia ukweli wote?*
- *Somo la Wakati na Biblia halijumuishi sehemu ya jinsi mishale ilivyotumiwa kama ishara ya kumjulisha Daudi kuhusu hatari aliyokuwa nayo. Unaweza kuongeza maelezo haya wanapotengeneza habari ya kuvutia.* Asubuhi iliyofuata Yonathani akaenda shambani ambako Daudi alikuwa amejificha nyuma ya mwamba. Alienda na mvulana. Mvulana alipiga mishale mitatu ikapita mbele yake. Tayari Daudi akajua kuwa ishara hiyo ilimaanisha kuwa maisha yake yako hatarini na kuwa alihitaji kukimbilia kwenye usalama. ***(1 Samweli 20:35-40)***
- Baada ya Yonathani kumwambia mvulana mwenye mishale arudi mjini, ilikuwa salama kwa Daudi na Yonathani kuwa na mazungumzo. *Jadili jinsi Daudi alivyojisikia kuhusu kuwa na rafiki kama Yonathani.* Ilikuwa vigumu kuagana, lakini waliahidiana kuwa watakuwa marafiki wakati wote. ***(1 Samweli 20:41-42)***
- *Zungumza jinsi Bwana Yesu alivyo Rafiki yetu kama tumemwalika katika maisha yetu kama Mwokozi. Tafakari juu ya kiwango cha upendo Wake katika kufa kwa ajili yetu na upendo Wake unaoendelea na wa uaminifu kila siku katika kutusaidia na kutulinda. Husianisha tena sifa za rafiki ambazo zilionyeshwa katika "Toa utangulizi".*

**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**
**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Daudi na Yonathani / Daudi akimbia asiuawe.

**JIFUNZE**

Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari Muhimu – ***1 Samweli 20: 17***

**KUMBUKA**

Kama una ubao wa dati unaowafaa watoto unaweza kuunganisha jaribio na wazo la mvulana aliyekuwa na mishale. Tumia maswali haya katika timu mbili:

- Sauli alitarajia Daudi awe wapi?
- Sauli alimkosa Daudi wakati gani?
- Sauli alitendaje kuhusu Daudi?
- Yonathani na Daudi walikutana wapi?
- Waliahidiana nini?
- Yesu anawezaje kuwa rafiki bora wa mtu?

## C7 Habari ya Pili

**Daudi aokoa maisha ya Sauli – Habari hii inahusu Daudi kumsamehe Sauli.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Daudi hakujaribu kulipiza kisasi kwa Sauli.<br>• Mungu anataka tufanye maamuzi sahihi kuhusu jinsi tunavyowatendea watu wengine.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Waefeso 4:32***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***1 Samweli 24:1-22*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Jadilini hali ambayo watoto wanakutana na mtu aliyewatendea mabaya. Je, wanajisikiaje? Je, wanapenda kulipiza kisasi? Jaribu kutumia mfano maalum wa hali ambayo watoto wanaweza kuhusianisha. Eleza kuwa kama Bwana Yesu ndiye Mwokozi wetu, atatusaidia kuchagua njia sahihi ya kuitikia na kusamehe wengine.<br>Katika habari ya leo, tutajifunza jinsi Daudi alivyomtendea mfalme Sauli. |
| **FUNDISHA** | *Rejelea Sauli alivyomtendea Daudi kwenye habari zilizopita (C6 Habari ya nne na C7 Habari ya kwanza).*<br><br>• *Elezea jangwa ambako Daudi alikuwa amejificha. Ongea juu ya mapango na jinsi yanavyoweza kuwa makubwa sana na yenye giza!* Sauli alikwenda kumtafuta Daudi akiwa na watu 3000. Kisha Sauli aliingia ndani ya pango lile ambalo Daudi alikuwa amejificha pamoja na watu wake. Jenga mashaka - Je, Sauli angempata Daudi? Sauli hakutambua kuwa Daudi alikuwa karibu sana nyuma ya pango ***(1 Samweli 24:1-3)***<br>• Watu wa Daudi waliona hii kama fursa kwa Daudi kujilipiza kisasi dhidi ya Sauli na walimhimiza Daudi amuue Sauli. *Wasaidie watoto kuchunguza chaguo ambalo Daudi alifanya. Je, ingekuwa sawa kwa Daudi kumuua Sauli? Elezea kuwa kwa wakati huo, Sauli alikuwa mfalme aliyetiwa mafuta na Mungu ingawa alifanya mambo mengi mabaya. Wakumbushe watoto kuwa Mungu alimwahidi Daudi kuwa angekuwa mfalme. Je, kuna kitu au mtu yeyote anaweza kubadilisha ahadi hiyo? Mungu alikuwa amemlinda Daudi hadi sasa - alipomuua Goliathi na baadaye Sauli alipojaribu kumuua kwa mkuki wake. Sisitiza kuwa maisha ya Daudi yalikuwa mikononi mwa Mungu, na hakuna mtu ambaye angeweza kuzuia ahadi na mipango ya Mungu kutekelezwa katika maisha yake. Daudi angekuwa mfalme katika wakati wa Mungu.* ***(2 Samweli 2:1-4)***<br>• Daudi alijua haingekuwa sawa kulipa kisasi kwa kumuua Sauli. *Eleza jinsi alivyosogea kwa siri mahali palipokuwa na kanzu ya Sauli na kukata upindo wa vazi lake!* Daudi alingoja hadi Sauli alipotoka pangoni. ***(1 Samweli 24:4-7)***<br>• Kisha Daudi akaenda hadi kwenye mlango wa pango na kumwita Sauli kwa sauti. *Tafakari mshangao ambao aliupata!* Daudi alimwonyesha Sauli upindo wa kanzu yake ambao alikuwa ameukata. *Sauli alitambua nini sasa?* Daudi alimweleza Sauli kuwa alikuwa ameokoa maisha yake. Moyo wa Sauli uliguswa. Alijua kuwa Daudi amekuwa mwema kwake na hakumtendea jinsi alivyostahili. Wakati huohuo, Sauli aliacha kumtafuta Daudi ili kujaribu kumdhuru. ***(1 Samweli 24:22)***<br>• *Jinsi Daudi alivyomtendea mfalme Sauli ni mfano wa jinsi Mungu alivyotutendea. Ametuonyesha rehema na msamaha wake ambao hatukustahili. Ametengeneza njia ili tupate kusamehewa kupitia kifo cha Bwana Yesu. Tunapomwamini Yesu na kusamehewa dhambi zetu, tunapaswa kufuata mfano wake na kuwa tayari kusamehe wengine.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Daudi Mfalme/Daudi aokoa Maisha ya Sauli |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na elezea Mstari Muhimu – ***Waefeso 4:32***. Mstari huu umegawanyika katika sehemu tatu ili watoto waweze kufanya mazoezi na kuigiza katika vikundi vya watu watatu. |
| **KUMBUKA** | Watoto wa Daraja la pili wanaweza kufanya kazi pamoja katika vikundi vidogo ili kutunga maigizo madogo kuhusu kusamehe wengine (angalia “Toa utangulizi”). Watoto wa Daraja la kwanza wanaweza kupamba herufi kubwa kuelezea maneno muhimu katika habari ya leo – mwenye huruma, mwema, anayesamehe. Zinaweza kuunganishwa kwenye kona kwenye kipande cha kitambaa kama njia ya kukumbusha habari ya leo. |

## C7 Habari ya Tatu

**Daudi awa Mfalme – Habari hii inahusu Mungu kutimiza ahadi Zake.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu alitimiza ahadi zake kwa Daudi kuhusu kuwa mfalme.<br>• Mungu alimpa Daudi ahadi nyingine kuhusu Mfalme mkuu zaidi.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***2 Samweli 5:4***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***1 Samweli 31:1-13, 2 Samweli 5:1-11*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza kuhusu jinsi ambavyo wakati mwingine tunalazimika kusubiri ahadi tulizoahidiwa kwa muda mrefu. Toa mfano ambao watoto wanaweza kuuelewa. Daudi anangoja kwa muda mrefu katika maishani yake. Rudia kile ambacho watoto tayari wanakijua kuhusu Daudi, kwa kuuliza maswali lakini uwe tayari kufafanua na kusimulia tena inapobidi. Je, Daudi alitoka katika familia ya kifalme? (yaani baba yake alikuwa mfalme?) Hapana, Daudi hakuwa mwana wa mfalme. Alitoka katika familia ya kawaida. Alifanya kazi gani? (alikuwa mchungaji) Ni nani aliyemchagua kuwa mfalme atakayefuata? (Mungu - alitiwa mafuta na nabii Samweli.) Sisitiza kuwa Daudi alikuwa chaguo la Mungu na Mungu angesababisha mpango wake utimie ingawa kulikuwa na mfalme mwingine wakati huo. Alikuwa nani? Sauli alifanya Daudi awe na wakati mgumu sana, lakini Daudi aliendelea kumtumaini Mungu |
| **FUNDISHA** | • Siku moja Sauli na familia yake waliuawa katika vita. Daudi alikasirishwa sana kuhusu kufa kwa Sauli ambaye mara nyingi alimtendea Daudi vibaya, na Yonathani mwana wa Sauli ambaye alikuwa rafiki mkubwa wa Daudi. ***(1 Samweli 31:1-6)*** Daudi aliandika shairi maalum la kumkumbuka Yonathani ***(2 Samweli 1:17-27)***<br>• Mara watu wakaja kwa Daudi. Kwa nini? Walimkumbusha Daudi jinsi alivyopaswa kuwa mchungaji wa watu wa Israeli na kuwa mtawala wao. *Linganisha usemi huu na maisha ya awali ya Daudi akiwa mchungaji.* Hatimaye ahadi ya Mungu kwa Daudi ilikuwa inatimia! Daudi alikuwa na umri wa miaka 30 alipoanza kuwa mfalme. Utawala wake ulidumu kwa miaka 40! ***(2 Samweli 5:1-5)***<br>• Kisha, Daudi aliurejeza tena mji wa Yerusalemu ambao ulikuwa umetwaliwa na maadui wa Mungu. Huko, Daudi alijenga jumba zuri la kifalme. Tunaambiwa kuwa Daudi alizidi kuwa na nguvu zaidi na zaidi kwa sababu Bwana Mungu Mwenyezi alikuwa pamoja naye. *Wafundishe watoto kuwa tunahitaji Mungu awe pamoja nasi pia.* ***(2 Samweli 5:9-11)***<br>• Daudi pia alikuwa tayari kujenga Hekalu ambapo Mungu angeweza kuabudiwa. *Elezea kuwa hadi sasa Mungu alikuwa anaabudiwa katika hema maalum lililoitwa Hema.* Lakini mmoja wa manabii wa Mungu, Nathani, alimpa Daudi ujumbe kuwa hii haikuwa sehemu ya mpango wa Mungu kwa Daudi. Kupitia Nathani, Mungu alimkumbusha Daudi mambo yote ya ajabu ambayo tayari alikuwa amemfanyia Daudi na kumpa ahadi nyingine ya ajabu kuwa mmoja wa familia ya Daudi angekuwa mfalme milele. *Waulize watoto kama wanaweza kujua huyu anaweza kuwa nani. (Toa vidokezo fulani kuhusu mtoto aliyezaliwa Bethlehemu au mfalme ambaye mamajusi walikuja kumtafuta) Wasaidie watoto watambue jinsi Daudi alivyolazimika kumsifu Mungu.* ***(2 Samweli 7)*** *Unaweza kusoma baadhi ya maneno ya Daudi ya sifa k.m.* ***mstari wa 22.***<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Daudi awa Mfalme |
| **JIFUNZE** | Mstari Muhimu ***2 Samweli 5:4*** ni taarifa ya uhakika kuhusu Daudi kuwa mfalme.<br>***Wagalatia 2:20*** ambayo inapatikana katika Daraja la kwanza na la pili katika somo la Wakati na Biblia ni muhtasari wa ajabu wa kile ambacho Bwana Yesu ametufanyia na ni vyema kuukariri. |
| **KUMBUKA** | Watoto wa Daraja la kwanza wanaweza kupamba mataji.<br>Maswali ya "Nani" hapa chini yanarejelea habari ya Daudi hadi sasa:<br>• Ni nani aliyemuahidi Daudi kuwa angekuwa mfalme?<br>• Ni nani alimtia mafuta Daudi katika nyumba ya baba yake?<br>• Daudi alimuua nani kwa kombeo?<br>• Ni nani alijaribu kumuua Daudi kwa mkuki?<br>• Ni nani alikuwa rafiki mkubwa wa Daudi?<br>• Ni nani alijificha kwenye pango?<br>• Nani walikufa vitani?<br>• Daudi alimsifu nani? |

## C7 Habari ya Nne

**Daudi na Mefiboshethi - Habari hii inahusu wema wa Daudi.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Daudi alitimiza ahadi zake kwa rafiki yake Yonathani katika kuonyesha wema kwa Mefiboshethi.<br>• Mungu ametuonyesha wema Wake.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***2 Samweli 9:7***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***2 Samweli 9:1-13*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Tumia hali zinazoeleweka kwa watoto ili kuwachochea kufikiria njia ambazo wanaweza kuonyesha wema kwa wengine k.m. ungeonyeshaje wema kwa: mtu aliyeanguka, aliyesahau kitu fulani, aliyebeba mizigo mingi, mwenye kazi nyingi za kufanya, asiye na mtu wa kucheza naye….? Katika mazingira ya shule, unaweza kuwauliza watoto waje na mifano yao wenyewe au unaweza kuelezea mifano ya watoto ambao wameonyesha wema kwa wengine siku hiyo. Katika habari ya leo, Daudi alitaka kupata mtu wa kumtendea wema. Pendekeza kuwa kutafuta njia za kuwa mwema kwa wengine ni jambo zuri kufanya! |
| **FUNDISHA** | • *Wakumbushe watoto kuhusu Habari ya 3 ambapo tulijifunza jinsi Mungu alivyotimiza ahadi zake kwa Daudi.* Sasa Daudi alikuwa mfalme na kulikuwa na amani. Lakini Daudi hakuwa amemsahau Yonathani rafiki yake mzuri na ahadi walizowekeana. *Taja kuwa ni jambo sahihi kutimiza ahadi ambazo tuliwaahidi wengine.* Daudi alijiuliza kama bado kuna mtu yeyote katika familia ya Yonathani ambaye angeweza kumtendea wema. Alimuuliza Siba ambaye alikuwa mmoja wa watumishi wa Mfalme Sauli kama alijua mtu yeyote. ***(2 Samweli 9:1-3)***<br>• *Mara moja Siba akamkumbuka Mefiboshethi. Rejea mambo yenye kuhuzunisha yaliyompata Mefiboshethi na ajali yake. Jinsi gani Mefiboshethi alijisikia alipokuwa anakua? Kuwa mwangalifu kama kuna watoto katika kikundi chako ambao wana hali ngumu na himiza kikundi chako kimshukuru Mungu kwa mambo mazuri waliyo nayo katika maisha yao.*<br>• *Sasa Mefiboshethi alikuwa akiishi mbali na Yerusalemu na bado hakuweza kutembea. Bashiri juu ya kile ambacho huenda alifikiria alipopokea mwaliko wa kwenda ikulu.* ***(2 Samweli 9:3-5)*** *Huenda aliogopa?*<br>• Mfalme Daudi alimweleza Mefiboshethi kuwa hana sababu ya kuogopa. Badala yake alitaka kumtendea mema. Alitaka kumwonyesha wema kwa ajili ya Yonathani na kwa sababu ya urafiki wa pekee ambao Daudi na Yonathani walikuwa nao. Daudi alikuwa mkarimu katika kile alichompa Mefiboshethi. *Unaweza kuorodhesha zawadi na fursa au kutumia picha rahisi kuwakilisha kila moja:*<br>*1) ardhi iliyokuwa mali ya Mfalme Sauli*<br>*2) watumishi wengi wa kulima ardhi*<br>*3) kuwa na sehemu katika meza ya mfalme*<br>• *Elezea kuwa kula pamoja na mfalme kulimaanisha kuwa alikuwa akitendewa kama mmoja wa familia ya mfalme.* Mefiboshethi alikubali kwa unyenyekevu kile alichopewa na Daudi, akitambua ukuu na wema wa Daudi. ***(2 Samweli 9:6-13)***<br>• *Habari hii inatusaidia kuelewa wema wa Mungu kwetu. Dhambi zetu hutuweka mbali na Mungu, lakini Mungu yuko tayari kuzisamehe na kutukaribisha katika familia yake. Hatustahili upendo kama huo, lakini Mungu anawezesha kupitia Mwanawe Bwana Yesu ambaye amekufa kwa ajili yetu. Wape changamoto watoto wakubali wema wa Mungu kwa kumshukuru kwa ajili ya Bwana Yesu.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Daudi na Mefiboshethi |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha Mstari Muhimu ambao ni sehemu ya habari kwenye Biblia au badala yake fundisha. ***Tito 3:4 "Lakini wema na upendo wa Mungu Mwokozi wetu ulipofunuliwa, alituokoa."*** |
| **KUMBUKA** | Watoto wa Daraja la pili wanaweza kufanya kazi katika vikundi kuunda bango ili kuonyesha njia ambazo Mungu anaonyesha wema kwetu. Watoto wa Daraja la kwanza wanaweza kufanya zoezi. Maswali yanaweza kuandikwa kwenye migongo ya picha za vitu vilivyowekwa kwenye meza ya mfalme na dondoo tofauti kwa ajili ya kila moja.<br>• Nani alikuwa Mfalme mwema?<br>• Nani alikuwa rafiki wa pekee wa Daudi?<br>• Nani alimwambia Daudi kuhusu Mefiboshethi?<br>• Nini kilimpata Mefiboshethi alipokuwa kijana?<br>• Daudi alimpa Mefiboshethi vitu gani viwili?<br>• Mefiboshethi alikula chakula chake wapi kuanzia sasa na kuendelea?<br>• Ni nani ametuonyesha wema?<br>• Jaza neno linalokosekana kutoka katika Mstari Muhimu "Lakini_________ na upendo wa Mungu Mwokozi wetu ulipofunuliwa, alituokoa. |

## C8 Habari ya Kwanza

**Yoshua awa kiongozi mpya - Habari hii inahusu kujua kwamba Mungu yuko pamoja nasi.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu aliahidi kuwa pamoja na Yoshua na kumsaidia.<br>• Mungu hutusaidia katika kazi anayotupa kufanya.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yoshua 1:9***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Yoshua 1:1-18*** |
| **TOA UTANGULIZI** | **Daraja la pili** - Waulize watoto ni nani anayesimamia shule yao au eneo lao jingine. Nini kitatokea kama mtu huyo hayupo? Nani atachukua nafasi yake, nani atakuwa msimamizi? (labda msaidizi wake)<br>Zungumza kuhusu jinsi ilivyo muhimu kuwa na mtu anayesimamia, anayefanya maamuzi na kuwajibika kwa ajili ya wale wote walio chini ya uangalizi wake. Kuwa mkuu na kutunga sheria kunaweza kuwa jambo la kufurahisha lakini onyesha wajibu ulivyo mkubwa wa kazi hiyo. Habari ya leo inahusu mtu mpya aliyepewa jukumu.<br><br>**Daraja la kwanza** – Jadili na watoto jinsi wanavyoweza kujisikia kuhusu kuchaguliwa kufanya jambo jipya na lenye changamoto. Toa mfano unaofaa. Katika habari ya leo Yoshua anapata kazi mpya. |
| **FUNDISHA** | • Mungu alizungumza na Yoshua na kumwambia kuwa Musa amekufa, na kwamba sasa angewaongoza watu kuingia katika Nchi ya Ahadi. ***(Yoshua 1:1-2)*** *Unadhani Yoshua alijisikiaje?*<br>• Watu walitakiwa kujiandaa kuvuka Mto Yordani na Mungu alikuwa anaenda kuwapa nchi ambayo alikuwa ameahidi miaka mingi iliyopita. Waisraeli walikuwa wamekaa hapa miaka 40 kabla ya hapo lakini walikuwa wametenda dhambi na hawakumwamini Mungu, kwa hiyo walikuwa wameachwa wakatangatanga jangwani. ***(Yoshua 1:3)*** *Zungumzia jinsi Waisraeli walivyojisikia. (msisimko, furaha, hamu, wasiwasi)*<br>• *Soma maneno ambayo Mungu alimwambia Yoshua katika mistari hii. Vuta usikivu wa watoto kwa jinsi Mungu anavyorudia maagizo Yake kuhusu kuwa hodari na moyo wa ushujaa. Je, hii ingemsaidiaje Yoshua kama kiongozi mpya? Eleza kuwa angeweza kuwa hivyo, si kwa sababu ya nguvu au uwezo wake mwenyewe bali kwa sababu Mungu alikuwa ameahidi kuwa pamoja naye.* ***(Yoshua 1:5-7, 9, 18)***<br>• Mungu pia alimkumbusha Yoshua kuhusu sheria na amri ambazo alikuwa amempa Musa. Yoshua alihitaji kujifunza na kuzitii. Kama angeshika amri za Mungu, Mungu angebariki watu katika makao yao mapya. ***(Yoshua 1:7-8)*** *Elezea kuwa ni muhimu sisi pia kumtii Mungu.*<br>• Kisha Yoshua akawaambia watu wote wabebe vitu vyao vyote na kuwa tayari kuondoka. Watu walimwahidi Yoshua kuwa kama walivyomtii na kumfuata Musa, wangemtii na kumfuata yeye pia. ***(Yoshua 1:10-11, 16-18)*** *Tunapomwamini Bwana Yesu na kumwomba aingie maishani mwetu, Yeye pia, ameahidi kuwa nasi na kamwe hatatuacha.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Yoshua awa kiongozi mpya |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na elezea Mstari Muhimu – ***Yoshua 1:9*** |
| **KUMBUKA** | Waambie watoto wajibu maswali yafuatayo kama njia ya kurejelea habari:<br>• Nani alikuwa amekufa?<br>• Mto waliopaswa kuvuka ulikuwa unaitwaje?<br>• Mungu alimwambia Yoshua alitakiwa kuwaje?<br>• Ahadi ya Mungu kwa Yoshua ilikuwa nini?<br>• Yoshua alihitaji kusoma na kujifunza nini?<br>• Watu walikubali kufanya nini? |

## C8 Habari ya Pili

**Yoshua na nchi mpya - Habari hii inahusu kuamini ukuu wa Mungu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Rahabu aliamini ukuu wa Mungu wa Israeli.<br>• Mungu anataka tuwe na imani kwake.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yoshua 2:24***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Yoshua 2:1-24*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Waulize watoto wanachojua kuhusu upelelezi. Jambo gani ni muhimu katika kuwa mpelelezi? Nini kinawapata wapelelezi wakikamatwa? Nini kingetokea kama ungekamatwa ukimsaidia mpelelezi ambaye anafanya kazi kwa ajili ya adui? |
| **FUNDISHA** | • Watu wawili walitumwa katika Nchi ya Ahadi kwenye mji mkubwa ulioitwa Yeriko. Walitakiwa kuipeleleza ili Waisraeli wajue jinsi ya kuteka nchi hiyo. Yeriko ulikuwa umezungukwa na ukuta mkubwa wenye malango ndani yake kwa ajili ya kuingilia mjini. Ukuta ulikuwa mnene kiasi kwamba kulikuwa na nyumba zilizojengwa juu yake. Mwanamke anayeitwa Rahabu aliishi katika mojawapo ya nyumba hizo.<br>• Watu hao walikwenda nyumbani kwa Rahabu. Kwa bahati mbaya, wapelelezi hao walionekana, na mfalme wa Yeriko akaambiwa. ***(Yoshua 2:1-2)*** *Waulize watoto watabiri nini kitatokea.*<br>• Mfalme alituma ujumbe kwa Rahabu awatoe watu hao, lakini Rahabu akawachukua watu hao na kuwaficha juu ya dari lake wakiwa wamefunikwa na majani. Aliwaambia wajumbe wa mfalme kuwa walikuwa wamechelewa sana, na watu hao walikuwa tayari wameondoka. Kisha askari wa mfalme wakatoka kwenda kujaribu kuwatafuta wapelelezi nje ya mji. ***(Yoshua 2:3-7)***<br>• *Wakati huohuo Rahabu aliwaambia wapelelezi kuwa nchi nzima inawaogopa Waisraeli. Walikuwa wamesikia yote ambayo Mungu alikuwa amefanya na walijua kuwa Mungu angewaangamiza. Rahabu aliwaomba wale wapelelezi kama wangeweza kumuokoa yeye na familia yake.* ***(Yoshua 2:8-13)*** *Elezea kuwa hilo lilionyesha kuwa Rahabu aliamini ukuu na nguvu za Mungu na kuwa alikuwa tayari kumtegemea Mungu ili awe salama. Hakuwa na fursa za kumjua Mungu kama Waisraeli walivyomjua lakini alikuwa tayari kuwa na imani katika Yeye. Kuwa na imani maana yake ni kumwamini au kumtegemea Mungu. Mungu anapendezwa tunapomuamini.*<br>• Wapelelezi waliahidi kumuokoa kama hatamwambia mtu yeyote kuwa walikuwepo pale. Walimwambia ahakikishe amefunga kamba nyekundu na kuining’iniza nje ya dirisha lake ndipo wote nyumbani kwake watakuwa salama. Kisha wapelelezi walishuka chini kwa kamba na kutoroka. (Onyesha kuwa nyumba ya Rahabu ilikuwa na dirisha lililoelekea nje ya mji). ***(Yoshua 2:14-21)***<br>• **Daraja la pili** – *Elezea kuwa kuna sura katika Agano Jipya ambapo watu wengi katika Biblia wametajwa kwa sababu ya imani yao. Soma* ***Waebrania 11:31.***<br>• Wale watu waliporudi kwa Yoshua, walitoa taarifa ya kile walichosikia, kuwa Mungu alikuwa pamoja nao, na kila mtu akawaogopa. Utume wao wa kupeleleza ulikuwa umewasaidia kuelewa zaidi kuhusu ukuu wa Mungu pia. ***(Yoshua 2:23-24)***<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Yoshua na nchi mpya |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari Muhimu – ***Yoshua 2:24*** |
| **KUMBUKA** | Waambie watoto wajibu maswali yafuatayo kama njia ya kurejelea habari:<br>• Yoshua alituma wapelelezi wangapi?<br>• Wapelelezi waliingia katika nyumba ya nani?<br>• Rahabu aliwaficha wapi wapelelezi?<br>• Aliwaomba wapelelezi wafanye nini?<br>• Wapelelezi walitorokaje?<br>• Walimwambia nini Yoshua? |

## <u>C8 Habari ya Tatu</u>
## Yoshua na Yordani- Habari hii inahusu nguvu za Mungu

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Hakuna jambo gumu ambalo Mungu haliwezi.<br>• Tunatakiwa kumtii Mungu, kwa chochote anachotuambia tufanye.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yoshua 3:5***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Yoshua 3:1-17, 4:1-24*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza na watoto kuhusu jambo ambalo wamewahi kuambiwa wafanye ambalo walidhani haliwezekani. Labda kazi ya nyumbani au kazi ya shuleni ambayo hawakuweza kuifanya. Je, walishughulikiaje tatizo lao? Je, kulikuwa na mtu mwingine ambaye aliweza kuwasaidia? Yoshua alihitaji kuwapeleka Waisraeli wote ng'ambo ya Mto Yordani. Ulikuwa ni mto mpana uliofurika na hapakuwa na madaraja wala mashua. Unadhani nani atamsaidia Yoshua? |
| **FUNDISHA** | • Yoshua na watu wote walifunga kambi yao na kuondoka kuelekea Yeriko. Walisimama kwenye ukingo wa Mto Yordani na kupiga kambi huko. ***(Yoshua 3:1)*** *Waambie watoto watafakari kuhusu kile ambacho watu walikuwa wanafikiria.*<br>• Baada ya siku tatu, Yoshua alituma ujumbe kuzunguka kambi ili kila mtu ajiandae kuondoka. Walitakiwa kuwafuata makuhani waliokuwa wamebeba Sanduku la Agano. (Hili lilikuwa sanduku maalum, takatifu ambalo liliwakumbusha kuwa Mungu alikuwa pamoja nao) Yoshua aliwaambia watu wajiandae kwa ajili ya siku inayofuata; Bwana alikuwa anaenda kuwatendea mambo ya ajabu. ***(Yoshua 3:2-5)***<br>• Yoshua aliwaambia makuhani watangulie mbele ya watu wote na walipaswa kutembea ndani ya Mto Yordani. Makuhani wakafanya kama Yoshua alivyosema, na mara miguu yao ilipogusa ukingo wa maji, mto ukaacha kutiririka na kulundikana na makuhani wakasimama mahali pakavu. (Unaweza kusema kuwa ardhi ilikuwa kavu na sio yenye unyevunyevu, licha ya ukweli kuwa maji yalikuwepo muda mfupi tu uliopita). ***(Yoshua 3:6-16)*** *Zungumzia jinsi watu walivyoitikia tukio hilo.*<br>• Kisha watu wote wakavuka mto ukiwa mkavu, wakaweza kupiga kambi ng'ambo ya mto, karibu na Yeriko. ***(Yoshua 3:17)***<br>• Mawe makubwa 12 yalichukuliwa kutoka Yordani na kuwekwa kando ya mto, kama ishara kwa siku zijazo ili waweze kukumbuka yale Mungu aliyowatendea siku hiyo. *Ni vyema tukumbuke nyakati ambazo Mungu ametusaidia.* Kila kitu kilipokamilika, Yoshua akawaamuru makuhani watoke mtoni. Mara tu miguu ya makuhani ilipogusa nchi kavu, mto ulianza kutiririka kama ulivyokuwa hapo awali. ***(Yoshua 4:1-9)***<br>• Kisha watu wakatambua kuwa Mungu alikuwa pamoja na Yoshua kama vile alivyokuwa pamoja na Musa. ***(Yoshua 4:14)*** *Tunapomwamini Bwana na kutii Neno Lake maishani mwetu, Yeye hutusaidia sikuzote.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A.- Yoshua na Yordani |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari Muhimu – ***Yoshua 3:5*** |
| **KUMBUKA** | Waambie watoto wajibu maswali yafuatayo kama njia ya kurejelea habari:<br>• Watu walipaswa kuvuka mto gani?<br>• Nani walitangulia kuingia mtoni?<br>• Walikuwa wamebeba nini?<br>• Nini kilitokea kwenye maji?<br>• Ni watu wangapi waliweza kuvuka?<br>• Walikusanya nini mtoni?<br>• Mawe yalikuwa ya nini?<br>• Walitambua nini kuhusu Yoshua? |

**C8 Habari ya Nne**

**Yoshua na Yeriko - Habari hii inahusu Mungu kuleta ushindi.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yoshua alifuata maelekezo ya Mungu ya kuteka mji wa Yeriko.<br>• Tunapaswa kumwamini na kumtii Mungu, kwa chochote anachotuomba tufanye.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Waebrania 11:30***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Yoshua 6:1-25*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Tuseme una jambo gumu sana la kufanya. Je, itasaidia:<br>• Kama utapewa maelekezo kamili na mtu anayeaminika?<br>• Kama mtu huyo pia atajitolea kwenda nawe ukiwa unaifanya kazi hiyo?<br><br>Hilo ndilo lililotukia wakati ulipowadia wa Waisraeli kuiteka Yeriko. |
| **FUNDISHA** | • *Wasaidie watoto kukumbuka jinsi Yeriko ilivyokuwa. Nani aliishi huko? (Habari ya 2)*<br>• Mungu alimwambia Yoshua kuwa Yeriko ilikuwa tayari kwa ajili yao kuivamia lakini haikuonekana kuwa iko tayari. Watu walikuwa wamefunga malango yote, na hakuna mtu aliyeruhusiwa kuingia au kutoka nje ya mji. Walijisikia kuwa salama kwa sababu ya ukuta mkubwa, mnene uliozunguka mji huo. ***(Yoshua 6:1)***<br>• Kisha Yoshua akawapa watu maelekezo aliyopokea kutoka kwa Mungu. Walitakiwa kuzunguka ukuta wa mji mara moja kila siku kwa siku sita. Mbele palikuwa na walinzi wenye silaha, kisha makuhani saba wenye tarumbeta za kondoo waume, kisha makuhani waliokuwa wakilichukua Sanduku la Agano, wakifuatiwa na walinzi nyuma yao. Watu walitakiwa kutembea wakiwa kimya huku tarumbeta zikipigwa. ***(Yoshua 6:2-11)*** *Je, Yoshua alikuwa na sababu yoyote ya kuogopa? Sisitiza kuwa kufuata mpango wa Mungu kungewafikisha kwenye ushindi wa hakika. Yoshua alikuwa na ahadi ya uwepo wa Mungu (Habari ya 1) na aliweza kutegemea nguvu na uaminifu wa Mungu. (Habari ya 3)*<br>• Kila siku watu waliamka mapema na kutembea mara moja kuzunguka mji. (Hali hii ingechukua muda mrefu – ulikuwa ni mji mkubwa. Pia elezea kuwa inawezekana watu wa Yeriko walikuwa juu ya ukuta wakiwatazama na pia kupitia madirishani. Kila siku, watu wengi zaidi walikuwa wakitazama madirishani, ili kuona maono haya ya ajabu ya watu wakizunguka kimya kimya) ***(Yoshua 6:12-14)***<br>• Ikafika siku ya saba. *Andaa mchezo wa kuigiza na matarajio ya ushindi ukisimulia jinsi walivyozunguka mji mara saba.* Makuhani walipopiga tarumbeta, Yoshua aliwaamuru watu wapige kelele. Watu walipopiga kelele kuta za Yeriko zilianguka na askari wakaingia ndani na kuwaua watu wote. ***(Yoshua 6:15-21)***<br>• Yoshua aliamuru wapelelezi wamtafute Rahabu na kumtoa yeye na familia yake nje ya mji hadi mahali salama. Yeye na familia yake yote waliokolewa na kuishi pamoja na Waisraeli tangu wakati huo na kuendelea. ***(Yoshua 6:22-23)***<br>• Yoshua aliwaamuru askari wasijichukulie dhahabu yoyote au fedha au vitu vingine vya thamani, bali wavilete kwenye Nyumba ya Mungu na kuviweka wakfu kwa Mungu. Askari na watu walijua kuwa si wao wenyewe waliomshinda adui bali ni Mungu. Mji uliharibiwa na kuteketezwa kabisa. ***(Yoshua 6:24-25)***<br>• Kwa hiyo, Mungu alimsaidia Yoshua na Waisraeli kuuteka mji mwovu wa Yeriko. Tunapomwamini Mungu anatusaidia kushinda yote ambayo ni mabaya katika maisha yetu.<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Yoshua na Yeriko |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari Muhimu – ***Waebrania 11:30*** |
| **KUMBUKA** | Waambie watoto wajibu maswali yafuatayo kama njia ya kurejelea habari :<br>• Yoshua na jeshi lake walijuaje wanalotakiwa kufanya?<br>• Watu wa Yeriko walikuwa wapi wakati jeshi lilipofika?<br>• Nini kilibebwa kuzunguka mji?<br>• Makuhani walipiga nini?<br>• Watu walizunguka mara ngapi kila siku?<br>• Walifanya hivi kwa siku ngapi?<br>• Walifanya nini siku ya saba?<br>• Nini kilifanya kuta zianguke?<br>• Nani aliokolewa?<br>• Nini kiliipata Yeriko? |

## <u>C9 Habari ya Kwanza</u>
## Eliya amtii Mungu - Habari hii inahusu kusikiliza na kufanya kile ambacho Mungu anasema.

<table>
<tr><td></td><td>Tunajifunza kuwa:<br>• Eliya alimtii Mungu alipompelekea Mfalme Ahabu ujumbe wa Mungu.<br>• Tunapaswa kutii yale ambayo Mungu anasema katika Biblia.<br><br>Mstari Muhimu: 1 Wafalme 17:5<br>Habari kwenye Biblia: 1 Wafalme 17:1-7</td></tr>
<tr><td>TOA UTANGULIZI</td><td>Waambie watoto waorodheshe mahitaji na matamanio yao na kutofautisha kati ya mambo hayo mawili.<br>Au mwombe mmoja ajitolee kujificha, au kuficha kitu, ili watoto watafute. Elezea kuwa mtu anayezungumziwa katika habari hii alijificha.</td></tr>
<tr><td>FUNDISHA</td><td>• Mfalme Ahabu hakumpenda Mungu na alikuwa mfalme mbaya zaidi katika Israeli kuwahi kutokea (ona 1 Wafalme 16:30). Aliabudu miungu ambayo haikuwa halisi na kuwafanya watu wa Israeli wafanye vivyo hivyo. Alikuwa amemuoa Malkia mwovu anayeitwa Yezebeli. Je, jambo hili lingemfanya Mungu ajisikieje? Mungu alikasirishwa na uovu wote katika nchi na alikuwa anaenda kumwadhibu Mfalme Ahabu. Mungu alimchagua Eliya, mtu aliyempenda Mungu, kuwa mjumbe wake. Alitakiwa kumwambia Ahabu kuwa hakutakuwa na mvua wala umande katika Israeli kwa muda mrefu. Soma maneno ya Eliya kwa mfalme (1 Wafalme 17:1). Eliya alimtii Mungu kwa kumwambia Mfalme Ahabu habari hizo mbaya.<br>• Unafikiri mfalme alijisikiaje kuhusu habari hii? Alikasirika. Jadili maana yake - mazao na mboga havingekua; wanyama na watu wasingekuwa na maji ya kunywa na chakula. Mfalme Ahabu alikasirika sana kwa sababu ya ujumbe wa Eliya kiasi kwamba alitaka kumuua! Lakini Mungu alikuwa na mpango wa kumweka Eliya salama. Akamwambia nenda kajifiche! Eliya alipaswa kusafiri hadi kwenye bonde lenye joto, lenye mwinuko lililoitwa Kerithi. Kulikuwa na kijito pale na Eliya angeweza kunywa maji hayo. Pia Mungu alisema angempa chakula kwa njia ya ajabu. Kila asubuhi na jioni, kunguru (ndege wakubwa, weusi) wangemletea Eliya mkate na nyama katika midomo yao. (1 Wafalme 17:2-4). Mungu alikuwa akimtunza Eliya. Eliya alitii na kuanza safari ya kuelekea bonde la Kerithi.<br>• Siku baada ya siku, Mungu alimpa Eliya mahitaji yake. Eliya alikunywa maji kutoka kwenye kijito na kunguru wakampa chakula. Kadiri muda ulivyopita, Eliya aligundua kuwa maji katika kijito yanakauka. Waulize watoto kama wanaweza kufahamu kwa nini. Kulikuwa hakuna mvua, kama Mungu alivyokuwa amesema. Maji yalipungua hadi siku moja kijito kikakauka. Eliya alipaswa kufanya nini sasa? Mungu tayari alikuwa na mpango kwa ajili ya Eliya! Alichopaswa kufanya ni kutii. (1 Wafalme 17:5-7).<br>• Eliya alimtii Mungu ingawa alijua kuwa kumwambia Mfalme Ahabu habari mbaya kungekuwa hatari kwake. Alimtii Mungu pia, akaenda hadi Kerithi ambapo Mungu alimpatia chakula na maji. Eliya alikuwa na ujasiri wa kufanya kile ambacho Mungu alimwambia afanye na aliamini Mungu atamtunza.<br>• Mungu anazungumza nasi leo kupitia Biblia. Anatuambia jinsi ya kuishi na jinsi ya kuwa mmoja wa watoto Wake. Tunahitaji kusikiliza yale ambayo Mungu anasema katika Biblia na kutii. Atawatunza na kuwajali wale wanaompenda.<br><br>Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.<br>Onesha: Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Eliya amtii Mungu</td></tr>
<tr><td>JIFUNZE</td><td>Kama inafaa, fundisha Mstari Muhimu na uuelezee: 1 Wafalme 17:5. Chagua sehemu ya kwanza ya mstari kwa ajili ya watoto wadogo.</td></tr>
<tr><td>KUMBUKA</td><td>Chora picha ya kitu kimoja kutoka kwenye orodha iliyotajwa katika utangulizi. K.m. chakula, maji, malazi, usafiri n.k. Zinaweza kufanywa onyesho lenye kichwa “Mungu hututimizia mahitaji yetu” au ZOEZI.<br>• Mfalme na malkia mwovu waliitwa nani?<br>• Mungu alikusudia kufanya nini ili kumwadhibu Mfalme Ahabu?<br>• Mungu alimchagua nani kumwambia mfalme mpango wa Mungu?<br>• Mfalme Ahabu aliitikiaje?<br>• Mungu alimtuma Eliya wapi?<br>• Mungu alimtunzaje Eliya huko?<br>• Hatimaye nini kilitokea kwenye kijito?<br>• Tunajifunza nini kuhusu Eliya kutokana na habari hii?<br>• Jinsi gani tunaweza kumtii Mungu ?</td></tr>
</table>

## C9 Habari ya Pili

**Eliya amtumaini Mungu - Habari hii inahusu Mungu kumpa Eliya yote anayohitaji.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Eliya na mjane walimwamini Mungu katika kuwapatia mahitaji yao.<br>• Mungu ameandaa njia kwa ajili ya hitaji letu la uzima wa milele.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Wafalme 17:14***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***1 Wafalme 17:8-24*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Tumia vielelezo vya wiki iliyopita na wape nafasi watoto wasimulie habari tena. Onesha kiasi kidogo cha unga kwenye ndoo, na mafuta kwenye jagi. Tungeweza kuoka nini? Onesha mkate. Je, ungewezaje kuoka mkate? (Joto kutoka kwenye oveni au moto) Onesha kitita cha vijiti. Elezea kuwa unga na mafuta vilikuwa kidogo sana. Vitu hivi viko katika habari ya leo. |
| **FUNDISHA** | • Mungu alimwambia Eliya aondoke Kerithi na kwenda katika mji uitwao Sarepta. *Simulia kile ambacho Mungu alimwambia Eliya pia kuwa mjane angempa chakula.* Waulize watoto maana ya mjane. Eliya alitii na kuanza safari ndefu yenye joto. Aliamini kuwa Mungu atamtunza. Alipofika kwenye mlango wa kuingilia mjini, alimuona mwanamke akiwa ameinama chini na kuokota kuni zilizoanguka kutoka kwenye matawi ya miti na vichaka. *Elezea mazungumzo katika **mistari ya 10-12**. Kwa nini mjane na mwanawe walikuwa na uhaba wa chakula?* Hapakuwa na mvua kwa hiyo mazao kwa ajili ya kupata unga hayakuwa yamepandwa. Watu walikuwa wanaenda kufa kwa kukosa chakula. ***(1 Wafalme 17:8-12)***<br>• *Husianisha kile Eliya alichomwambia mwanamke, na kile ambacho Mungu aliahidi **(mistari ya 13-14)**. Unafikiri mwanamke huyo alifanya nini?* Mwanamke alitumaini na kuamini kuwa Mungu angetimiza ahadi yake. Alienda kumtengenezea Eliya mkate mdogo, kisha akajitengenezea mwenyewe na mwanawe. Kitu cha kushangaza kilitokea! Alipotazama kwenye pipa la unga, unga bado ulikuwa umesalia na kulikuwa na mafuta ndani ya chupa. Unga na mafuta vingeweza kuisha. Lakini siku baada ya siku, pipa lilikuwa na unga ndani yake na chupa ya mafuta haikuisha kamwe. Ilikuwa kama Mungu alivyosema! Kulikuwa na chakula kila siku kwa ajili ya Eliya, mwanamke na mwanawe. Mungu alikuwa ametimiza ahadi yake. Aliwapa mahitaji yao. ***(1 Wafalme 17:13-16)***<br>• *Sehemu ya mwisho ya kifungu cha Biblia* ***(1 Wafalme 17:17-24)*** *imetajwa tu katika Daraja la 2 la Wakati wa Biblia.* Jambo la kusikitisha, siku moja kijana mdogo wa mwanamke huyo aliugua sana akafa. Akambeba mtoto mikononi mwake hadi kwa Eliya. Alimchukua mtoto huyo hadi chumbani kwake na kumlaza kitandani. Eliya alisali mara tatu: “Ee BWANA, Mungu wangu, mfufue mtoto huyu.” Mungu alisikia sala ya Eliya na mtoto huyo akaanza kupumua tena! Akambeba yule mtoto mpaka chini na kumpa mama yake. Mungu alikuwa ameonyesha nguvu na wema Wake mkuu kwa mwanamke mjane, mwanawe na Eliya! Mungu hakuwa amewaandalia tu chakula chao cha kila siku, bali alikuwa amemfufua mwana wa mjane. Mwanamke huyo alijua kuwa Mungu wa Eliya ndiye Mungu wa kweli.<br>• *Mungu hutupatia mahitaji yetu leo - chakula, familia, na marafiki. Lakini pia tunahitaji jambo muhimu zaidi. Tunahitaji Mungu atusamehe dhambi zetu - makosa tunayofanya. Mungu alimtuma Mwana wake, Yesu, afe ili tupate kusamehewa dhambi zetu. Tukiomba, Mungu atatusamehe dhambi zetu, na tutapata uzima wa milele. Jadilini hii ina maana gani.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Eliya amtumaini Mungu |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari Muhimu – ***1 Wafalme 17:14***.<br>*Elezea kuwa Mungu alitimiza ahadi yake. Anatimiza ahadi zake zote katika Biblia.* |
| **KUMBUKA** | Katika vikundi vya watatu igizeni ***1 Wafalme 17:10-16***<br>• Mungu alimwambia Eliya aende wapi wakati kijito cha Kerithi kilipokauka?<br>• Alimwona nani alipofika huko?<br>• Mwanamke alikuwa anafanya nini?<br>• Aliomba nini?<br>• Jibu la mwanamke lilikuwaje?<br>• Ahadi ya Mungu kwa mwanamke ilikuwa nini?<br>• Mungu alitimizaje ahadi hii?<br>• Maswali ya **DARAJA LA PILI** Nini kilimpata mwana wa mjane?<br>• Eliya aliomba mara ngapi?<br>• Ni nguvu ya nani iliyomrudishia mtoto uhai wake?<br>• Tunahitaji nini zaidi ya yote? |

## C9 Habari ya Tatu

**Eliya amtumikia Mungu - Habari hii inahusu Mungu kumpa Eliya ushindi.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu alimpa Eliya ushindi kwenye shindano la Mlima wa Karmeli.<br>• Mungu wa Biblia ndiye Mungu wa kweli.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Wafalme 18:39***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***1 Wafalme 18:1-2, 16-46*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Elezea mashindano ni nini kwa kutumia mifano, kama vile michezo kati ya timu mbili. Zungumza kuhusu uchaguzi tunaofanya kila siku - rangi unazopenda, chakula, muziki. Watu katika habari yetu wanatakiwa kufanya chaguo muhimu sana. |
| **FUNDISHA** | • Mvua haikunyesha kwa miaka mitatu mizima katika Israeli. *Elezea hii ingemaanisha nini - hakuna mazao, nyasi, mboga mboga, lakini pia wanyama na watu wangekufa. Wakumbushe watoto kwa nini Mungu aliwaadhibu watu wa Israeli kwa njia hii - uovu wa Mfalme Ahabu na ibada ya miungu ya uongo.* Mungu alimwambia Eliya arudi kwa Mfalme Ahabu na kumwambia kuwa siku za karibuni Mungu angeleta mvua. Eliya alitii. ***(1 Wafalme 18:1-2)***<br>• Mfalme Ahabu bado alikuwa na hasira na Eliya. Alikuwa ametishia kumfanya nini? (kumuua). Safari hii alimwita Eliya mtaabishaji. *Elezea jibu la Eliya katika **mstari wa 18**.* Ilikuwa wakati wa kuthibitisha ni nani aliyekuwa Mungu wa kweli. Eliya alianzisha mashindano ambayo yangefanywa kwenye Mlima wa Karmeli unaoelekea baharini. *Elezea kilichotokea katika mstari wa 19 na 20 na changamoto ambayo Eliya aliwapa watu katika **mstari wa 21**.* ***(1 Wafalme 18:16-21)***<br>• Mashindano hayo yangekuwa kati ya mungu wa uwongo Baali na Mungu wa kweli. *Elezea jinsi ambavyo madhabahu mbili zingejengwa, na dhabihu kuwekwa juu ya kila moja. Wale waliomwamini Baali na Eliya aliyemwamini Mungu wa kweli kila mmoja angeomba moto ushuke na kuteketeza dhabihu kwenye madhabahu yao. Popote ambapo moto ungeshuka, ingethibitisha ni nani aliyekuwa Mungu wa kweli.* ***(1 Wafalme 18:22-26)***<br>• Wafuasi wa Baali walisali kwanza. Waliomba asubuhi yote, lakini hapakuwa na jibu kutoka kwa mungu wao, hakuna moto ulioshuka. Walipiga kelele kwa nguvu zaidi, hakuna aliyejibu, *Waulize watoto kama wanaweza kujua kwa nini?* Walikuwa wakiomba miungu ya mawe isiyoweza kusikia. ***(mistari ya 25-29)*** Sasa ilikuwa zamu ya Eliya. Dhabihu ilipowekwa juu ya madhabahu, Eliya alimimina mapipa 12 ya maji juu yake. *Kwa nini? Jambo hili lingefanya iwe vigumu kwa moto kuteketeza dhabihu.* Eliya aliomba kwa utulivu kwa Mungu wa Israeli. *Simulia maombi yake katika **mistari ya 36 na 37**.* Mara moja, moto kutoka kwa Mungu ulishuka na kuteketeza dhabihu, mawe ya madhabahu na kukausha maji. Mungu Aliye Hai alikuwa amesikia maombi ya Eliya na kuonyesha nguvu zake kuu. Watu walipoona yaliyotukia, walianguka chini na kulia: “BWANA ndiye Mungu.” ***(mistari ya 38-39)*** Eliya aliamuru manabii wa Baali wauawe. ***(Mstari wa 40)***<br>• Ni ushindi ulioje kwa Eliya na Mungu wake! *Eliya alikuwa amemuahidi nini Ahabu mwanzoni mwa habari yetu?* Kama Mungu alivyoahidi, anga likawa jeusi kwa mawingu, upepo ukavuma, na mvua kubwa ikanyesha. ***(1 Wafalme 18:41-46)***<br>• Watu wa Israeli waliona siku hiyo kuwa Mungu ndiye Mungu wa pekee wa kweli. *Wakumbushe watoto kuwa Eliya alisema nini katika **mstari wa 21**.* Waliacha kuabudu miungu ya uongo na kurudi kumwabudu Mungu wa kweli. *Watu wengi leo wanaabudu miungu ya uwongo. Mungu wa Biblia ndiye Mungu wa kweli. Je, uko tayari kumpa Mungu wa kweli nafasi ya kwanza maishani mwako na kumpokea Mwanawe, Yesu, kuwa Mwokozi na Bwana wako?*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Eliya amtumikia Mungu |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari Muhimu – ***1 Wafalme 18:39***. |
| **KUMBUKA** | Waambie watoto wasimulie tena habari kwa kutumia vielelezo au watumie maswali ya zoezi.<br>1. Ni ujumbe gani kutoka kwa Mungu ambao Eliya alimpa Mfalme Ahabu?<br>2. Mfalme Ahabu alimwitaje Eliya?<br>3. Eliya alijibu nini?<br>4. Watu walitakiwa kufanya chaguo gani? ***(mstari wa 21)***<br>5. Nini kilitokea wakati watu waliomwamini Baali walipoomba?<br>6. Eliya alifanyaje ili iwe vigumu zaidi kwa moto kuteketeza dhabihu?<br>7. Nini kilitokea Eliya alipoomba?<br>8. Watu walifanyaje na walisema nini?<br>9. Ni ahadi gani nyingine ambayo Mungu alitimiza mwishoni mwa habari? |

**C9 Habari ya Nne**

**Eliya ashindwa kumtumaini Mungu – Habari hii inahusu mtu aliyeogopa na kumsahau Mungu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Eliya alipoogopa, alisahau kumwamini Mungu kuwa atamtunza.<br>• Tunaweza kumtumaini Mungu kila wakati.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Zaburi 62:8***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***1 Wafalme 19:1-16*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Jadili njia ambazo Mungu amemsaidia Eliya katika habari hizi hadi sasa:<br>1) Kumpa mahali salama pa kujificha<br>2) Kumlinda dhidi ya Mfalme Ahabu<br>3) Kumpa chakula<br>4) Kuonyesha nguvu Zake dhidi ya waabudu Baali.<br>Je, unadhani ingekuwa rahisi kwa Eliya kumwamini Mungu kuanzia sasa na kuendelea? |
| **FUNDISHA** | • Mke wa Mfalme Ahabu, Malkia mwovu Yezebeli, alikasirika aliposikia jambo lililotokea kwenye Mlima wa Karmeli kwamba manabii wa Baali walikuwa wameuawa kwa maagizo ya Eliya. *Rejea habari ya Mlima wa Karmeli kama haijatumiwa katika utangulizi.* Watu wa Israeli walikuwa wamejifunza nini? Mungu wa Eliya alikuwa Mungu wa kweli. Kwa hasira yake, Malkia Yezebeli alituma ujumbe kwa Eliya akisema kuwa angemuua siku hiyo kwa kile alichokifanya. Eliya aliposikia hivyo, aliogopa na kukimbia ili kuokoa maisha yake! Alihisi upweke na huzuni na akasahau kumwamini Mungu. *Zungumza na watoto kuhusu nyakati ambapo wanahisi huzuni na upweke, wanapodhihakiwa shuleni au kuingia kwenye mabishano.* Mungu anajua yote yanayotokea na yanayotufanya tuhuzunike na kuogopa. ***(1 Wafalme 19:3)***<br>• Eliya alikimbilia kwenye jangwa lenye joto na vumbi na kuketi chini ya mti. Alimwomba Mungu amruhusu afe kisha akalala. *Waambie watoto kuhusu riziki iliyotolewa na malaika.* Mungu huwajali wale wanaompenda. Baada ya kula na kulala, Eliya alikuwa na nguvu za kutosha kutembea kwa siku 40 mchana na usiku hadi Mlima Horebu (unaoitwa pia Mlima Sinai). *Waulize watoto kama wanaweza kukumbuka chochote kilichotokea pale – Musa alipewa na Mungu amri 10. Eliya alikaa usiku kucha katika pango.* ***(1 Wafalme 19:3-9)***<br>• *Husianisha swali ambalo Mungu alimuuliza Eliya na jibu lake.* Eliya aliweza kumwambia Mungu jinsi alivyojisikia na kwa nini alikuwa na huzuni sana. Daima Mungu anasikiliza. Unaweza kumwambia jinsi unavyojisikia na kwa nini una huzuni au hofu. *Toa utangulizi wa Mstari Muhimu -* ***Zaburi 62:8 (1 Wafalme 19:9-10)***<br>• Mungu alimwambia Eliya aende na kusimama mlimani. Mungu alikuwa anaenda kukutana na Eliya. Kukaja upepo mkali, tetemeko la ardhi na moto, lakini Mungu hakuzungumza na Eliya katika mojawapo ya vitu hivi. Kisha Eliya akasikia sauti ya utulivu. Alikuwa ni Mungu akizungumza. Akamwambia Eliya arudi kwa njia aliyokuja nayo. Husianisha kile Mungu alichosema na kazi mpya alizokuwa nazo kwa ajili ya Eliya. Mungu bado alikuwa tayari kumtumia Eliya kama msaidizi wake ingawa alikuwa ameogopa na kusahau kumwamini. Mojawapo ya kazi ambayo Mungu alikuwa nayo kwa Eliya ilikuwa ni kutafuta kijana aliyeitwa Elisha ambaye angekuwa nabii au mjumbe wa Mungu. Eliya alikuwa mzee na maisha yake yalikuwa yanakaribia mwisho. Alikuwa amemtumikia Mungu vizuri. ***(1 Wafalme 19:11-16)***<br>• *Mungu alikuwa amezungumza na Eliya katika maisha yake yote na kumwambia mambo anayotakiwa kufanya. Mungu anazungumza nasi leo kupitia yale tunayosoma katika Biblia. Ukiwa na huzuni au woga, mwombe Mungu awe nawe na akusaidie. Unaweza kumwamini Mungu kila wakati.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Eliya ashindwa kumtumaini Mungu/Eliya aomba tena/ amsahau Mungu |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari Muhimu – ***Zaburi 62:8***. Mungu habadiliki. Anapatikana kila wakati kwa ajili yetu. |
| **KUMBUKA** | Watoto wanaweza kuchora au kuunda kalenda ya matukio ya habari, au zoezi:<br>• Ni nani aliyetishia kumuua Eliya?<br>• Eliya alifanyaje alipotishiwa?<br>• Alimwomba Mungu amruhusu afanye nini?<br>• Malaika alimpa chakula gani?<br>• Ilichukua muda gani kwa Eliya kufika kwenye Mlima Horebu?<br>• Mungu aliuliza swali gani na Eliya alijibu nini?<br>• Taja vitu vitatu ambavyo Mungu hakuvitumia kuzungumza na Eliya?<br>• Mungu alizungumzaje na Eliya?<br>• Alimpa kazi gani?<br>Je, unazungumza na Mungu ukiwa na huzuni au hofu? |

**C10 Habari ya Kwanza**

**Elisha – wito wa kufuata – Habari hii inahusu Mungu kuwa pamoja nasi.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu alimpa Elisha uwezo wa kufanya kazi Yake.<br>• Mungu atawasaidia wote wanaompenda na kumtumikia.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***2 Wafalme 2: 14***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***1 Wafalme 19: 19-21, 2 Wafalme 2: 1-15*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Jadili njia ambazo watu humtumikia Mungu - wamisionari, wahudumu wa kanisa, mashirika ya Kikristo ya kutoa misaada, kuwaambia wengine kuhusu Yesu.<br>*Zungumza na watoto kuhusu mambo ambayo ni magumu kwao kuyafanya - kazi zao za shule, kuweka akiba ya pesa zao za matumizi, kutokuwa na hasira, nk.* Wakati mwingine tunahitaji msaada kutoka kwa watu wengine. Huyu mtu katika habari yetu alihitaji msaada wa Mungu katika kufanya kazi ambayo Mungu alikuwa amempa. |
| **FUNDISHA** | • Ni nani ambaye Mungu alikuwa amemchagua kuchukua nafasi ya Eliya ili awe mjumbe Wake mpya? Rejea maagizo ya Mungu kwa Eliya katika ***1 Wafalme 19:15-16***. Eliya alijua kwamba kazi yake kwa Mungu ilikuwa inakaribia mwisho, kwa hiyo aliondoka Mlima Horebu ili kumtafuta Elisha, kijana mdogo ili kuendeleza kazi ya Mungu. Eliya alimkuta Elisha akilima shambani *(onyesha picha za jinsi kulima kulivyofanywa nyakati za Biblia)*. Akavua vazi lake na kulitupa juu yake. Elisha alijua hii ilikuwa ishara kwamba alikuwa amechaguliwa na Mungu kuacha kazi yake ya ukulima na kumtumikia Mungu. Aliaga familia yake na kwenda na Eliya kuanza kazi yake mpya. ***(1 Wafalme 19:19-21)***<br>• Eliya na Elisha walienda kila mahali pamoja walipokuwa wakimtumikia Mungu. *(Kama muda unaruhusu, husianisha na **2 Wafalme 2:1-6**), ukikazia kwamba Elisha aliazimia muda wote kuwa na Eliya.* Baada ya muda, watu hao wawili wakafika kwenye ukingo wa mto Yordani. Eleza kilichotokea katika mstari wa 8. Eliya aliweza kufanya hivyo kwa sababu Mungu alikuwa pamoja naye na alimpa nguvu. Eliya alimuuliza Elisha alichotaka amfanyie kabla hajachukuliwa na Mungu. Elisha alijua kwamba angehitaji nguvu zilezile alizokuwa nazo Eliya ili kumsaidia kufanya kazi ya Mungu. *Husianisha na mazungumzo katika* **2 Wafalme 2:7-10**.<br>• Ghafla jambo la kushangaza lilitokea walipokuwa wakizungumza. Gari na farasi wa moto vilitokea kati ya watu hao wawili. Eliya aliinuliwa juu kuelekea Mbinguni katika upepo mkali wa kisulisuli. Elisha hakuweza tena kumwona Eliya, isipokuwa vazi lake lililokuwa limeanguka chini. *Waulize watoto jinsi Elisha alivyojisikia (upweke, mshangao, na huzuni)* ***(2 Wafalme 2:11-12)***<br>• Elisha aliliokota vazi na kurudi mtoni. Elisha alijiuliza kama Mungu alikuwa pamoja naye. *Eleza Elisha alivyolitumia vazi na kile kilichotokea.* ***(mstari wa 14)*** Elisha alijua sasa kwamba Mungu wa Eliya alikuwa pamoja naye na angempa nguvu alizohitaji kufanya kazi yake kwa ajili ya Mungu. Mungu angemsaidia kama alivyomsaidia Eliya. ***(2 Wafalme 2:13-15)***<br>• *Hata leo Mungu hutumia watu kufanya kazi yake. Anaweza kukutaka uende nchi nyingine au ubaki katika nchi yako. Mungu anataka wale wote wanaompenda wamtumikie. Tunaweza kumtumikia Mungu kwa njia zipi? Mifano ni pamoja na kuwa mkarimu kwa wengine, kuwaalika marafiki kwenye Shule ya Jumapili, au kuwaambia wengine kuhusu Yesu. Tunamtumikia Mungu kwa kuishi maisha yanayompendeza. Chochote unachomfanyia Mungu, atakusaidia - kama vile alivyowasaidia Eliya na Elisha.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Elisha: wito wa kufuata. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari Muhimu – ***2 Wafalme 2: 14***. Zingatia maneno ya Elisha na ueleze mazingira ya tukio. |
| **KUMBUKA** | Chora mchoro wa gari na watoto walipambe kwa miali ya moto - rangi, crayoni, karatasi ya rangi, au zoezi:<br>• Eliya alitakiwa kumtafuta nani ili achukue nafasi yake kwa ajili ya kumtumikia Mungu?<br>• Elisha alikuwa akifanya nini Eliya alipokutana naye?<br>• Elisha alifanya nini?<br>• Ni nani alisababisha mto Yordani ugawanyike ili watu wavuke?<br>• Elisha aliomba nini?<br>• Ni nini kilitokea kati ya Eliya na Elisha wakati Eliya alipoinuliwa kwenda Mbinguni?<br>• Elisha aliokota na kutumia kitu gani?<br>• Je, sasa Mungu alikuwa pamoja na Elisha? Elisha alijuaje?<br>• Nani atakusaidia katika kazi yako kwa ajili ya Mungu? |

## <u>C10 Habari ya Pili</u>

**Elisha – faraja kwa ajili ya rafiki – Habari hii inahusu nguvu ya Mungu juu ya kifo.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Maombi ya ya Elisha yalimfufua mwana wa mwanamke.<br>• Tunaweza kumuomba Mungu kuhusu mambo magumu maishani mwetu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***2 Wafalme 4: 33***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***2 Wafalme 4: 8-37*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Je, umewahi kumsaidia rafiki? Jadilini. Utaona watu wakisaidia marafiki zao katika habari hii. Au ungeweka nini kwenye chumba cha kulala kwa ajili ya rafiki zako? Wangehitaji nini? Mwanamke anajenga chumba cha kulala kwa ajili ya rafiki katika hii habari yetu. |
| **FUNDISHA** | • Elisha alizunguka nchi nzima akifanya kazi ya Mungu. *Rejea jinsi Elisha alivyochukua nafasi ya Eliya na alivyopewa na Mungu uwezo wa kufanya hivyo.* Mara nyingi alitembelea mahali paitwapo Shunemu ambapo mwanamke mmoja tajiri aliishi pamoja na mume wake. Walipenda kumkaribisha Elisha nyumbani kwao kwa ajili ya chakula, na baada ya muda waliamua kumjengea chumba chake juu ya nyumba yao ambapo angeweza kulala usiku. *Eleza walichoweka katika chumba cha kulala - kitanda, kiti, meza, na taa. Wanandoa hao walionyesha wema kwa rafiki yao. Tunapaswa kufanya vivyo hivyo kwa marafiki zetu.* ***(2 Wafalme 4:8-10)***<br>• Elisha alitaka kufanya jambo fulani kwa ajili ya wema wao. Alisikia kwamba mwanamke huyo alikuwa na huzuni kwa sababu hakuwa na watoto. Elisha alimwambia kwamba Mungu angempa mtoto wa kiume! Muda si muda mwanamke huyo alipata mtoto wake wa kiume. *Unadhani alijisikiaje? (furaha)*. Siku moja ya huzuni, mvulana huyo alipokuwa mkubwa na kumsaidia baba yake shambani, aliugua sana. Alibebwa hadi ndani ya nyumba lakini mara akafa. *Unadhani mama yake alimfikiria nani ambaye angeweza kusaidia? (Elisha).* Alijua Elisha alikuwa mtu wa Mungu na angeweza kumsaidia kwa nguvu za Mungu. Akauweka mwili wa mwanawe juu ya kitanda cha Elisha, akapanda punda na kwenda nyumbani kwa Elisha. *Unapokuwa na shida unamgeukia nani ili akusaidie? (wazazi, mwalimu, kaka au dada)* ***(2 Wafalme 4:11-25)***<br>• *Kwa kundi la umri huu, matukio yafuatayo yamerahisishwa.* Elisha akarudi na yule mwanamke na kwenda chumbani kwake ambapo mwili wa mvulana umelazwa. Alifunga mlango na kumwomba Mungu. Alipuliza pumzi yake ndani ya mwili wa mvulana huyo na mvulana huyo akaanza kupata uhai. Ghafla, alipiga chafya mara saba na kufumbua macho yake. Mungu alikuwa amejibu maombi ya Elisha! Akamrudisha mvulana kwa mama yake. Bila shaka alifurahi sana kumwona mwanawe akiwa hai! Elisha alimwamini Mungu kuwa atamsaidia, na Mungu akajibu maombi yake. Mwanamke, mume wake na mvulana walijifunza kuhusu nguvu za Mungu siku hiyo. ***(2 Wafalme 4:26-37)***<br>• *Jambo hili la ajabu lilitokea kwa sababu Elisha alimwomba Mungu. Mungu anataka tumwamini na kuomba kwa ajili ya mambo magumu katika maisha yetu. Jadilini aina mbalimbali za mambo magumu - rafiki anapohama, mbwa anapokufa, mtu fulani anapokusumbua shuleni. Mungu atasikiliza maombi yetu na anaweza kutusaidia. Mungu anawajali wale wanaompenda. Hivyo atakuwa pamoja nao katika shida zao.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Elisha: faraja kwa ajili ya rafiki. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari Muhimu – ***2 Wafalme 4:33.*** |
| **KUMBUKA** | Watoto wanaweza kuchora picha za hali ambayo wanaweza kuiombea au kufanya zoezi:<br>• Mwanamke tajiri na mume wake walimtunzaje Elisha?<br>• Mungu alimuahidi nini mwanamke?<br>• Mungu alitimizaje ahadi Yake?<br>• Mvulana alipougua alikuwa wapi?<br>• Mama yake aliuweka wapi mwili wake?<br>• Ni nani alienda kutafuta msaada?<br>• Elisha alifanya nini aliporudi nyumbani kwake?<br>• Mungu alijibuje maombi yake?<br><br>Tunapaswa kufanya nini tunapokuwa na huzuni au wasiwasi? |

## C10 Habari ya Tatu

**Elisha – kuponya mwenye ukoma – Habari hii inahusu upendo wa Mungu kwa kila mtu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Naamani alikuwa na ugonjwa ambao ungeweza tu kuponywa na Mungu.<br>• Mungu amefanya njia ili tupate kusamehewa tatizo la dhambi.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***2 Wafalme 5: 15***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***2 Wafalme 5: 1-19*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Unaenda kumuona nani ili akutibu unapokuwa mgonjwa? Jadilini. Huyu mtu katika habari yetu alikuwa mgonjwa na hakuna mtu aliyeweza kumsaidia.<br>Au zungumza kuhusu maelekezo, kwa maandishi na kwa maneno. Huyu mtu katika habari yetu alipaswa kutii maelekezo yaliyotolewa na Elisha, ingawa hakutaka. |
| **FUNDISHA** | • Naamani, jemadari wa jeshi la Mfalme wa Aramu, alikuwa mtu muhimu sana. Alikuwa mwanajeshi shujaa, alikuwa ameshinda vita vingi na mfalme alifurahishwa naye sana. Aliishi katika nyumba kubwa na mke wake na watumishi. Lakini alikuwa adui wa watu wa Mungu, yaani Waisraeli. Siku moja, jambo baya lilitokea. Aliitazama ngozi yake na kuona kuna kitu kibaya. Alikuwa na ukoma - ugonjwa ambao siku hizo haukuweza kuponywa na madaktari. Baada ya muda mfupi, watu wengine wangemwona ana ugonjwa huo. Angepoteza kazi yake na kufukuzwa akakae mbali na familia yake. *Jadilini jinsi ambavyo Naamani angejisikia kama angeambiwa hivyo.* ***(2 Wafalme 5:1)***<br>• Nyumbani kwake kulikuwa na mjakazi mdogo ambaye alimhudumia na kumsaidia mke wake. Alikuwa ametekwa kutoka katika nchi ya Israeli na kununuliwa nyumbani kama mtumishi. Alisikia habari mbaya kuhusu Naamani na alijua mtu ambaye angeweza kusaidia. *NANI? (Husianisha na* ***mstari wa 3****)* Naamani alikubali kwenda kumwona Elisha. Ukoma ulikuwa tatizo ambalo Naamani hangeweza kulitatua. *Tuna shida ambayo hatuwezi kuitatua - dhambi ambayo inatufanya tutende mambo mabaya.* Mfalme wa Aramu alimruhusu Naamani kwenda kumwona Elisha na akampa dhahabu, fedha na mavazi ili achukue kama zawadi. ***(2 Wafalme 5:2-7)*** *Naamani alijisikiaje sasa?*<br>• Naamani alipofika, Elisha alimtuma mjumbe kumwambia akaoge mara saba katika mto Yordani kisha atapona ukoma wake. Naamani alikasirika - alikasirika kwamba Elisha hakuwa ametoka mwenyewe kumwona na vilevile hakutaka kuoga kwenye mto wa Yordani wenye matope. *Eleza jinsi watumishi wa Naamani walivyomshawishi afuate maelekezo ya Elisha.* ***(mstari wa 13)*** *Watoto wa Daraja la 1 wanaweza kuhesabu mara ngapi Naamani alijichovya kwenye maji kwa kusimama, kuinama na kuinua mwili wake tena. Ni jambo la ajabu sana, Naamani aliponywa! Ngozi yake ilionekana iko sawa. Simulia kile ambacho Naamani alimwambia Elisha.* ***(mstari wa 19)*** Naamani sasa alijua Mungu wa Israeli ndiye Mungu wa kweli. Naamani alimpa Elisha zawadi za dhahabu, fedha na mavazi mazuri, lakini Elisha hakuzipokea. Mungu ndiye aliyekuwa amemponya Naamani, na sio Elisha. ***(2 Wafalme 5:8-19)***<br>• *Naamani alipaswa kutii kile ambacho Elisha alisema ili aponywe ukoma wake. Haikuwepo njia nyingine ya yeye kuponywa. Mungu ametutengenezea njia ili tatizo letu la dhambi litatuliwe. Dhambi hututenganisha na Mungu. Katika Biblia, Mungu anatuambia kwamba kwa sababu Mwana wake, Yesu, alikufa msalabani, tunaweza kumwomba Mungu atusamehe dhambi zetu. Hakuna njia nyingine ya sisi kusamehewa dhambi zetu. Kisha tunakuwa sehemu ya familia ya Mungu. Je, umemwomba Mungu akusamehe dhambi yako? Atakusamehe kama utamuomba.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Elisha: kuponya mwenye ukoma / kutakasa mwenye ukoma. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari Muhimu – ***2 Wafalme 5: 15***. Zingatia maneno yaliyonenwa na Naamani - Mungu wa Israeli ndiye Mungu wa kweli. |
| **KUMBUKA** | Daraja la 1 - Mwambie kila mtoto achore uso wa huzuni na madoa upande mmoja na uso wa furaha bila madoa upande mwingine wa sahani ya karatasi. Zitumie hizo picha kusimulia tena habari:<br>• Naamani alifanya kazi gani?<br>• Alikuwa na ugonjwa gani?<br>• Ni nani alimwambia Naamani kuhusu Elisha?<br>• Ni nani alimruhusu Naamani aende kumwona Elisha?<br>• Naamani alichukua zawadi gani?<br>• Naamani alitakiwa kuoga kwenye mto Yordani mara ngapi?<br>• Naamani alfanyaje alipoambiwa aoge kwenye mto Yordani?<br>• Ni nani walimwambia atii maelekezo ya Elisha?<br>• Ni nini kilitokea Naamani alipotoka majini baada ya mara ya saba?<br>• Alimwambia nini Elisha?<br>• Kwa nini Elisha hakuwa tayari kupokea zawadi?<br>• Ni tatizo gani tulilo nalo ambalo ni Mungu pekee awezaye kulitatua? |

<u>**C10 Habari ya Nne**</u>

**Elisha – kudanganya kwaadhibiwa – Habari hii inahusu kusema ukweli.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu alimwadhibu Gehazi kwa kuwa na tamaa mbaya na kusema uwongo.<br>• Yesu alichukua adhabu ya dhambi zetu alipokufa msalabani.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Hesabu 32: 23***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***2 Wafalme 5: 19-27*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Jadilini maana ya kuwa na tamaa mbaya ya vitu. Au je ni jambo jema kusema uwongo? Tunapofanya mambo haya, tunadhani kwamba hakuna mtu atakayejua au kugundua kama alivyofanya huyu mtu kwenye habari hii.<br>Onyesha picha na/au zoezi ili kurejelea habari ya Naamani. Hiki ndicho kilichotokea baadaye. |
| **FUNDISHA** | • *(Rejea kisa cha Naamani, kama hakijatumiwa katika utangulizi.)* Naamani, jemadari wa jeshi, watu wake na watumishi wake wakaondoka kurudi nyumbani. Naamani alifurahi kwamba alikuwa ameponywa ukoma wake na sasa alijua kwamba Mungu wa Elisha alikuwa Mungu wa kweli. Lakini kulikuwa na mtu ambaye hakuwa na furaha. *(Huyo mtu anaweza kuwa ni nani?)* Gehazi, mtumishi wa Elisha alikasirika kwamba bwana wake hakukubali zawadi za fedha na nguo nzuri kutoka kwa Naamani. *Je, unaweza kukumbuka kwa nini Elisha hakuchukua zawadi alizopewa? Mungu ndiye alimponya Naamani na sio Elisha.* Gehazi alifikiri ni upumbavu kwa Elisha kutochukua chochote kutoka kwa Naamani na alipanga kujipatia baadhi ya zawadi. Gehazi alikuwa na tamaa mbaya. Gehazi alikosea kwa kusema uwongo ili kupata alichotaka. ***(2 Wafalme 5:19-20)***<br>• Gehazi alikimbia kumfuata Naamani ingawa alikuwa ameshaenda umbali fulani katika safari yake. Naamani alipomwona Gehazi akikimbia nyuma yao, alishuka kwenye farasi wake na kumuuliza Gehazi kama kuna shida yoyote. Simulia jibu la Gehazi katika ***mstari wa 22***. Gehazi alikuwa ametunga hadithi ambayo haikuwa ya kweli ili kujipatia fedha na mavazi mazuri. Mungu amesema tusiseme uwongo. *Rejea* ***Kutoka 20:16***. Gehazi alimdanganya Naamani ili ampe zawadi zilizokusudiwa kwa ajili ya Elisha. Naamani alimpa Gehazi zaidi ya alivyokuwa ameomba! Alituma watumishi wake wawili wamsaidie kubeba zawadi hizo kurudi nyumbani kwa Gehazi. *Sisi pia tumevunja Amri za Mungu na wakati mwingine tunasema uwongo ili kutoka kwenye tatizo au kupata kitu ambacho si chetu.* ***(2 Wafalme 5:21-23)***<br>• Watumishi walimpa Gehazi zawadi na Gehazi akazificha nyumbani kwake. Alidhani hakuna mtu angejua alichokuwa amefanya. *Unadhani alikuwa sahihi? Nani angejua alichokuwa amefanya? Mungu! Mungu anajua tunapofanya mambo mabaya. Anajua kila kitu. Hafurahii tunapodanganya au kusema uwongo.* ***(2 Wafalme 5:24)***<br>• Gehazi akaenda kwa Elisha na kusimama mbele yake. Eleza mazungumzo yao katika ***mistari 25-26***. Eleza kwamba Mungu alikuwa amemwambia Elisha kile ambacho mtumishi wake alikuwa amefanya. Mungu alimwadhibu Gehazi kwa kosa alilofanya. Hakuweza kukwepa. Dhambi zake zilikuwa zimejulikana kwa Mungu. Ghafla Gehazi akawa amefunikwa na ukoma. ***(2 Wafalme 5:25-27)***<br>• *Biblia inasema sote tunafanya mambo mabaya. Sisi sote tumetenda dhambi. Mungu anajua yote tuliyofanya. Tunaweza kumwomba Mungu atusamehe dhambi zetu kwa sababu Mwanawe, Yesu, alichukua adhabu ya dhambi alipokufa msalabani. Je, umemwomba Mungu akusamehe dhambi yako?*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki / kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Elisha: kudanganya kwaadhibiwa. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari Muhimu – ***Hesabu 32: 23***. Eleza kwamba baadhi ya watu wanafikiri kwamba hakuna mtu atakayejua kuhusu dhambi zao, lakini Mungu anajua kila kitu. Mungu atawaweka wazi. |
| **KUMBUKA** | Waambie watoto wajibu maswali yafuatayo kama njia ya kuirejelea habari:<br>• Kwa nini Gehazi alidhani Elisha, bwana wake, alikuwa mjinga?<br>• Gehazi alifanya nini?<br>• Alimwambia Naamani nini?<br>• Je, unaweza kumwelezeaje Gehazi?<br>• Ni nani aliyemsaidia Gehazi kurudi nyumbani kwake na zawadi kutoka kwa Naamani?<br>• Gehazi alizifanyia nini zawadi?<br>• Je, alidhani hatajulikana? Nani alijua?<br>• Ni nini kilimpata Gehazi?<br>• Tunaweza kufanya nini kuhusu dhambi zetu, au mambo tunayofanya vibaya? |

## C11 Habari ya Kwanza

**Yona ndani ya merikebu – Habari hii inahusu Mungu kujua kila kitu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yona hakutii na alijaribu kujificha mbali na Mungu.<br>• Mungu anataka tumtii.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yona 1: 3***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Yona 1: 1-9*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza na watoto kuhusu njia mbalimbali tulizonazo za kuwasiliana sisi kwa sisi - maandishi, simu, barua, barua pepe n.k. Jadili jinsi Mungu anavyowasiliana nasi. Biblia ni Neno la Mungu. Tunapoisikiliza au kuisoma, Roho Mtakatifu huleta ujumbe wake maishani mwetu.<br>Waelezee watoto kwamba katika nyakati za Agano la Kale Mungu alituma neno lake kupitia kwa wanadamu, wanaoitwa manabii. Watu hawa walitumwa na Mungu sehemu mbalimbali ili kupeleka ujumbe wa Mungu kwa watu walioishi huko. |
| **FUNDISHA** | • Mungu alizungumza na nabii aliyeitwa Yona na kumwambia aende Ninawi. Palikuwa mbali sana na mahali alipokuwa akiishi Yona. *(Maili 500 - toa maoni yako kuhusu umbali huu ulivyokuwa mrefu.)* Watu wa Ninawi hawakumjua Mungu na waliishi maisha ya dhambi. Kazi ya Yona ilikuwa kuwaambia kwamba Mungu atawaadhibu kama hawatamgeukia na kutubu. *(kujutia dhambi zao kwelikweli) Tafakari jinsi Yona alivyojisikia alipoambiwa afanye hivyo - woga, upweke n.k.* ***(Yona 1:1-2)***<br>• Yona aliamua kukimbilia upande mwingine na kujaribu kujificha mbali na Mungu. *Jadilini kama inawezekana kujificha mbali na Mungu, ikizingatiwa kwamba Yeye yuko kila mahali na anaweza kutuona kila wakati.* Yona alikwenda Yafa ambako alipanda merikebu iendayo Tarshishi. ***(Yona 1:3)***<br>• *Elezea upepo wa kutisha uliotumwa na Mungu - sauti za upepo na mawimbi yakiipiga merikebu, pia vitu vikirushwa huku na huku.* Mabaharia waliogopa sana na kuomba miungu yao. *Eleza kwamba kwa vile hawakumjua Mungu mmoja wa kweli, maombi yao hayakujibiwa. Wakiwa wamekata tamaa walijaribu kupunguza uzito wa merikebu kwa kutupa mizigo baharini.* Yona alikuwa amelala fofofo chini na hakujua kinachoendelea. Nahodha akamuamsha na kumwambia amwite Mungu wake aiokoe merikebu. ***(Yona 1:4-6)***<br>• Mabaharia waliamini kwamba dhoruba hiyo ilisababishwa na kosa la mtu aliyekuwa kwenye merikebu. *Eleza jinsi walivyopiga kura ili kumjua kwa kutumia kete au majani.* Kura ilimuangukia Yona! Walimuuliza Yona kuwa yeye ni nani na ametoka wapi. Yona alieleza kwamba alikuwa Mwebrania, ambaye alimtumikia Mungu wa Mbinguni, aliyeumba bahari na nchi kavu na vyote vilivyomo. Aliwaambia dhoruba imekuja kwa sababu ya kosa lake kwa sababu alikuwa akimkimbia Mungu. ***(Yona 1:9)***<br>• *Eleza kwamba tunaposoma Biblia na kujifunza kile ambacho Mungu anataka tufanye, tunapaswa kutii ujumbe wake na tusifanye kama Yona alivyofanya.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Yona ndani ya merikebu. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari Muhimu – ***Yona 1:3*** |
| **KUMBUKA** | Waambie watoto wajibu maswali yafuatayo kama njia ya kurejelea habari:<br>• Yona alikuwa anafanya kazi gani?<br>• Mungu alitaka Yona aende wapi?<br>• Kwa nini Yona hakutaka kwenda huko?<br>• Yona alijaribu kufanya nini?<br>• Ni nini kilitokea merikebu ilipoanza safari?<br>• Yona alikuwa akifanya nini wakati wa dhoruba?<br>• Mabaharia waligunduaje kwamba lilikuwa kosa la Yona?<br>• Yona alisema kuwa alikuwa anamtumikia nani? |

**C11 Habari ya Pili**

**Yona baharini – Habari hii inahusu jinsi Mungu anavyojibu maombi.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu alijibu maombi ya Yona akiwa ndani ya samaki.<br>• Mungu atasikia maombi yetu tukimlilia.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yona 2: 9***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Yona 1: 10-17 & 2: 1-10*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Ongea juu ya hali ambapo vitendo vya mtu vinaweza kumuweka yeye mwenyewe na watu wengine hatarini. k.m shuleni, mmoja akiwa na utovu wa nidhamu anaingiza darasa zima kwenye matatizo, mtu akiendesha gari bila uangalifu, mtu asiyefuata ushauri wa afya.<br>Wakumbushe watoto kuhusu Yona na jinsi kutotii kwake kulivyosababisha kila mtu ndani ya merikebu kuwa hatarini. |
| **FUNDISHA** | • Mabaharia walipogundua Yona ni nani na alimtumikia nani waliogopa sana. Walimuuliza Yona wafanye nini ili kuzuia upepo huo mkali usiwaangamize. Yona aliwaambia kuwa upepo huo umesababishwa na kosa lake, kwa vile alikuwa akijaribu kumkimbia Mungu, kwa hiyo wamtupe baharini. Hata hivyo, watu hao hawakutaka kumuua Yona, kwa hiyo walijaribu kupiga makasia kurudi pwani, lakini upepo ulizidi kuwa mkali. Kisha mabaharia walimlilia Mungu na kuomba kwamba wasiadhibiwe kwa kumuua Yona. Wakamnyanyua Yona na kumtupa baharini. Mara huo upepo ukakoma, na bahari ikatulia. Watu waliokuwa kwenye merikebu walitambua Mungu alikuwa nani na wakamtolea sifa na ibada zao. ***(Yona 1:10-15)***<br>• Yona alipozama, Mungu alituma samaki mkubwa ambaye alikuja na kummeza. *Wasaidie watoto watafakari jinsi Yona alivyokuwa ndani ya samaki.* ***(Yona 1:17)***<br>• Yona alifanya jambo pekee lililowezekana! Alimuomba Mungu. *Zungumzia jinsi Mungu anavyosikia maombi yetu bila kujali mahali tulipo.* Katika sala yake Yona alizungumza kuhusu kile ambacho Mungu alikuwa amemfanyia tayari. Alikumbuka jinsi alivyodhani atakufa alipokuwa akizama chini ya bahari. Alikumbuka jinsi alivyomlilia Mungu na jinsi Mungu alivyosikia maombi hayo na kuokoa maisha yake. Alimshukuru Mungu kwa kumsikia na kukiri kwamba Mungu ndiye Mungu pekee wa kweli na kwamba watu wanaoomba sanamu hawataweza kuokolewa na miungu yao. Yona alimsifu Mungu kwa kuwa ndiye Mungu pekee anayeweza kuokoa. ***(Yona 2:1-9)***<br>• Baada ya siku tatu mchana na usiku ndani ya tumbo la samaki, Mungu aliamuru samaki amtapike Yona kwenye nchi kavu. ***(Yona 2:10)***<br>• Mungu alimwadhibu Yona kwa kutotii kwake, lakini pia aliandaa njia ya kumwokoa (samaki) wakati alipojutia na kutambua dhambi yake. *Tunastahili kuadhibiwa kwa ajili ya dhambi zetu, lakini Mungu amefanya njia ili tupate kusamehewa kupitia yale ambayo Bwana Yesu amefanya. Kama ilivyokuwa kwa Yona, sisi pia tunapaswa kujutia dhambi zetu. Mungu yuko tayari kutuokoa na dhambi zetu tunapomwomba.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Yona baharini. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee – ***Yona 2:9.*** |
| **KUMBUKA** | Waambie watoto wajibu maswali yafuatayo kama njia ya kurejelea habari:<br>• Mabaharia walifanya nini kwanza Yona alipowaambia wamtupe baharini?<br>• Kwa nini hawakutaka kumtupa Yona baharini?<br>• Ni nini kilitokea walipomtupa Yona baharini?<br>• Mabaharia walifanya nini walipoona upepo umekoma?<br>• Mungu alituma nini ili kumwokoa Yona?<br>• Yona alikuwa ndani ya tumbo la samaki kwa muda gani?<br>• Yona alifanya nini alipokuwa ndani ya samaki?<br>• Ni somo/masomo gani ambayo Yona alijifunza?<br>• Tunafananaje na Yona?<br>• Inawezekanaje Mungu kutuokoa? |

## C11 Habari ya Tatu

**Yona ahubiri Ninawi – Habari hii inahusu kumgeukia Mungu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Watu wa Ninawi walitubu kweli kweli na wakasamehewa na Mungu.<br>• Tunahitaji kutubu dhambi zetu ili kusamehewa na Mungu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yona 3: 5***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Yona 3: 1-10*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza na watoto kwamba:<br>1) mara ngapi wamelazimishwa kuomba msamaha wakati hawakumaanisha kabisa.<br>2) mara ngapi walijua wamefanya makosa.<br>3) waeleze kuhusu hatia na nafuu waliyopata walipoomba msamaha.<br>Jadili kama inawezekana mtu kuonyesha kwa vitendo au kwa tabia kuwa ametubu. Leo tutaangalia jinsi watu wa Ninawi walivyotubu. |
| **FUNDISHA** | • Mara tu Yona alipotoka kwenye samaki, ndipo Mungu alipozungumza naye tena, akimwambia aende Ninawi kupeleka ujumbe wa Mungu. Wakati huu Yona alimtii Mungu mara moja. Ninawi ulikuwa ni mji mkubwa sana kiasi kwamba ilichukua siku tatu kuuzunguka. Yona alianza kuwaambia watu kwamba Mungu angewaangamiza kwa sababu ya njia zao mbaya. ***(Yona 3:1-4)***<br>• Cha kushangaza watu waliamini ujumbe wa Yona na kuchukizwa sana na kile walichokifanya. Walitaka kumwonyesha Mungu jinsi walivyojutia. Walifunga (wakaacha kula) na kuvaa nguo za magunia badala ya nguo zao za kawaida. Hii ilikuwa njia yao ya kuonyesha jinsi walivyojiona kuwa hawana thamani na kutubu kweli. ***(Yona 3:5)***<br>• Habari zilipomfikia mfalme, alishuka kutoka kwenye kiti chake cha enzi, akavua mavazi yake ya kifalme na kuvaa nguo za magunia pia. Akatoa amri kwamba kila mtu mjini, ikiwa ni pamoja na wanyama wote, wasile chochote na wavae nguo za magunia. Pia aliamuru kwamba kila mtu aache njia zake mbaya na kumlilia Mungu. Mfalme alitumaini kwamba Mungu angewaona na kuwasikia watu na kisha kutotekeleza mpango wake wa kuwaangamiza. ***(Yona 3:6-9)***<br>• Mungu aliona kwamba watu walikuwa wamejuta kweli kweli, walikuwa wameacha dhambi zao, na hawakuwa wakifanya maigizo, kusudi waweze kuokoa maisha yao wenyewe. Walikuwa tayari kubadilika, kuacha kabisa njia zao mbaya na kumgeukia Mungu. Biblia inatumia neno **tubu** kuelezea walichofanya. Mungu alibadilisha mawazo yake juu yao, kwa kuwasamehe na sio kuwaangamiza.<br>• *Eleza kwamba Mungu bado ni mwenye fadhili na anasamehe leo. Kama walivyokuwa watu wa Ninawi, tukimrudia Mungu, na kutubu dhambi zetu, na kuamini ujumbe Wake, tutaokolewa.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Yona ahubiri Ninawi. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa,fundisha na uelezee Mstari Muhimu – ***Yona 3:5*** |
| **KUMBUKA** | Waambie watoto wajibu maswali yafuatayo kama njia ya kurejelea habari:<br>• Mungu alitaka Yona afanye nini sasa?<br>• Ilichukua muda gani kuzunguka mji wa Ninawi?<br>• Ni mambo gani mawili ambayo watu walifanya ili kuonyesha kwamba walijutia dhambi zao kwelikweli?<br>• Mfalme alifanya nini ili kuonyesha kuwa alijutia?<br>• Mfalme aliwaamuru watu wafanye nini?<br>• Mungu aliamua kufanya nini?<br>• Tunatakiwa kutubia nini?<br>• Mungu atatufanyia nini tukitubu? |

## C11 Habari ya Nne

**Yona kivulini – Habari hii inahusu upendo na huruma ya Mungu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Habari ya Yona inatuonyesha mfano wa kile alichofanya Yesu.<br>• Mungu anawapenda na kuwajali watu wote.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 12: 41***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Yona 4: 1-11*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza na watoto kuhusu jinsi gani, na wakati gani tunapowaza kuhusu mtu fulani aliyefanya jambo baya, tunavyotaka kuona akiadhibiwa. Wakati mwingine tunaweza kumwambia mzazi au mwalimu tunapomwona mtu akifanya jambo baya na kisha tunaweza kukasirika wakati tunapodhani hakuadhibiwa kama ilivyopaswa. Hivi ndivyo Yona alivyohisi kuhusu Mungu katika habari ya leo. |
| **FUNDISHA** | • Ingawa Yona alikuwa amemtii Mungu mara ya pili kwa kwenda Ninawi, alikuwa na hasira kwamba Mungu alikuwa amewasamehe watu. Alijua kwamba Mungu ni mwenye rehema, si mwepesi wa hasira na amejaa upendo, lakini alikasirika kwamba Mungu aliwatendea hivyo watu wa Ninawi. Yona bado alikuwa na masomo ya kujifunza! ***(Yona 4:1-3)***<br>• Yona alitoka nje ya mji na kuketi akitazama kama Mungu atafanya jambo lolote. Ilikuwa siku yenye joto sana. *Waulize watoto wanajisikiaje joto likiwa kali sana na nini kingewasaidia.* Mungu alitimiza hitaji la Yona kwa kusababisha mmea wenye majani ukue ili kumlinda jua lisimuunguze. Usiku huo Yona alilala chini ya kivuli chake. ***(Yona 4:5-6)***<br>• Kulipopambazuka siku iliyofuata, Mungu akatuma mdudu kuushambulia mmea. Mara, ukanyauka na kufa. Kisha Mungu akatuma upepo mkali na jua likamchoma Yona kama hapo awali. *Alijisikiaje sasa? Eleza kwamba kwa mara ya pili, alikuwa na hasira na Mungu, wakati huu kuhusu mmea.* Kisha Mungu akazungumza na Yona kuhusu kuhangaikia kwake mmea ambao hata hakuwa ameupanda na ambao ulikuwepo kwa muda mfupi tu. Mungu alieleza kwamba alikuwa na haki kubwa zaidi ya kuwajali watu wa Ninawi. Kulikuwa na watu 120,000 *(pengine ulinganishe na idadi ya watu wa mahali fulani ambapo watoto wanapajua)* ambao walihitaji kujua njia za Mungu. Ndiyo maana aliwapa nafasi ya kutubu. Wote walikuwa muhimu kwa Mungu na hakuna hata mmoja aliyekuwa mbaya sana kiasi cha kutokustahili upendo wa Mungu! *Jadili jinsi fikra za Yona kuhusu watu wa Ninawi na mmea zilivyokuwa za kichoyo ilhali alihitaji kuelewa moyo wa Mungu wa upendo kwa wanadamu.* ***(Yona 4:7-10)***<br>• *Mungu anawapenda na kuwajali watu wote, haijalishi wako mbali kiasi gani katika kutii njia zake. Ni muhimu kwamba kila mtu ulimwenguni apate nafasi ya kusikia habari njema kuhusu Bwana Yesu.*<br>• Eleza kwamba Yesu alipokuwa duniani alizungumza na watu kuhusu Yona. Aliwaambia kwamba angezikwa kwa muda wa siku tatu mchana na usiku, muda kama uleule ambao Yona alikuwa ndani ya samaki. Pia aliwaambia kwamba watu wa Ninawi wangewakasirika watu waliosikia habari za Yesu bila kumwamini, kwa sababu walikuwa wamesikia ujumbe kutoka kwa Yona, wakausikiliza na kutubu. Yesu alikuwa mkuu zaidi kuliko Yona hivyo ni lazima tumwamini. ***(Mathayo 12:40-41)***<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Yona amwomba Mungu. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari Muhimu – ***Mathayo 12:41*** |
| **KUMBUKA** | Waambie watoto wajibu maswali yafuatayo kama njia ya kurejelea habari:<br>• Kwa nini Yona alimkasirikia Mungu?<br>• Yona alitaka nini kitokee kwake mwenyewe?<br>• Yona alienda wapi?<br>• Mungu alituma nini ili kumsaidia Yona?<br>• Mmea ulipata kitu gani?<br>• Kwa nini Yona alikasirika?<br>• Tunajifunza nini kuhusu jinsi Mungu alivyohisi kuhusu watu wa Ninawi?<br>• Habari ya Yona inaendana vipi na yale yaliyompata Yesu? |

## C12 Habari ya Kwanza

**Mungu amtuma Mwanawe, Yesu – Habari hii inahusu kuzaliwa kwa Yesu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu Mwana wa Mungu alizaliwa Bethlehemu.<br>• Yesu alizaliwa kuwa Mwokozi wa ulimwengu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Yohana 4: 14***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Luka 2: 1-7*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Onyesha watoto baadhi ya picha za watoto. (Ikiwezekana, lete picha yako ukiwa mtoto mchanga au waambie watoto walete picha zao wakiwa watoto wachanga.) Jadilini mahali ambapo kwa kawaida watoto huzaliwa kama vile hospitali na jinsi wanavyotunzwa wanapozaliwa mfano, jinsi unavyowavalisha, unavyowalaza nk. Eleza kwamba leo watajifunza habari kuhusu mtoto aliyezaliwa katika mazingira tofauti kabisa. |
| **FUNDISHA** | • Mtawala wa Kirumi alitaka kujua ni watu wangapi walikuwepo kwenye utawala wake. Aliagiza kila mtu arudi mahali alipozaliwa ili wahesabiwe. ***(Luka 2:1-3)***<br>• Yusufu na Mariamu waliishi Nazareti. Walikuwa wachumba wanaotarajia kuoana. Mariamu alikuwa anatarajia kupata mtoto siku za karibuni. Kwa Yusufu na Mariamu, ilimaanisha kwamba walitakiwa kufunga safari kutoka Nazareti hadi Bethlehemu ***(Luka 2:4-5)*** *Eleza umbali (angalau maili 80) na kwa Daraja la 2, tumia ramani ikiwa inapatikana. Watoto wanaweza pia kufikiria ni wapi familia zao zingelazimika kwenda kama agizo hili lingetolewa katika nyakati zetu hizi.*<br>• Walipokuwa Bethlehemu, mtoto akazaliwa. Mariamu akamvika mtoto wake nguo za kitoto, akamlaza katika hori ya kulia ng'ombe kwa sababu hapakuwa na nafasi katika nyumba ya wageni. *Eleza kwamba hori ilikuwa mahali ambapo wanyama walipatumia kwa kula na kisha mjadiliane kama palikuwa mahali pazuri pa kulaza mtoto mchanga (rejea mjadala wa utangulizi).* ***(Luka 2:6-7)***<br>• *Eleza kwamba ingawa mtoto huyu, Mwana wa Mungu, alikuwa mtoto wa pekee zaidi kuwahi kuzaliwa katika ulimwengu huu, Alizaliwa katika hali ngumu na alikulia katika familia maskini. Mungu alionyesha jinsi anavyotupenda kwa kumtuma Mwanawe ulimwenguni na siku moja mtoto huyu mdogo angekua na kufa msalabani kama Mwokozi wa ulimwengu. (Angalia Mstari Muhimu)*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Mungu amtuma Mwanawe, Yesu. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari Muhimu – ***1 Yohana 4:14.*** |
| **KUMBUKA** | Waambie watoto wajibu maswali yafuatayo kama njia ya kurejelea habari:<br>• Ni nani aliyekuwa akitawala nchi wakati huo?<br>• Mfalme alimwambia kila mtu afanye nini?<br>• Yusufu alikuwa anatarajia kumuoa nani?<br>• Yusufu na Mariamu waliishi wapi?<br>• Walilazimika kusafiri kwenda wapi ili kuhesabiwa?<br>• Ni nini kilikuwa kitu cha kipekee kwa mtoto aliyezaliwa?<br>• Mariamu alimvika nini?<br>• Mariamu alimweka wapi? |

## C12 Habari ya Pili

**Mungu amtuma Yesu, Mwokozi – Habari hii inahusu malaika kuwatokea wachungaji.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Wachungaji walikuwa watu wa kwanza kuambiwa kwamba Yesu amezaliwa.<br>• Malaika walitangaza kuwa Yesu ni nani.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 2: 11***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Luka 2: 8-15*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza na watoto kuhusu majina. Waulize kama wanajua kwa nini walipewa majina hayo, au kama kuna mtoto mchanga katika familia zao. Zungumza kuhusu familia, na kuhusu sababu za uchaguzi wa jina. Waulize watoto kama wamewahi kuitwa kwa majina mengine yoyote tofauti na yale waliyopewa yaani majina ya utani. Wakumbushe watoto kuhusu habari iliyotangulia kuhusu kuzaliwa kwa Mwana wa Mungu. Waambie watoto kwamba mtoto huyo alipewa jina la Yesu lakini pia alipewa majina mengine ya kipekee sana. |
| **FUNDISHA** | • Karibu na Bethlehemu kulikuwa na wachungaji fulani huko kondeni, wakichunga kondoo zao usiku. ***(Luka 2:8)*** *Eleza kwa nini ilikuwa lazima kwa wachungaji kuwachunga kondoo wao usiku. Eleza pia kwamba pengine walikuwa watu pekee waliokuwa macho ambao wangeweza kusikia habari hizi njema.*<br>• Kulitokea nuru kuu katika anga na malaika akatokea. *Waulize watoto wanadhani wachungaji walikuwa na matarajio gani. (kuogopa, kushangaa, kushtuka)*. Malaika akawaambia, “Msiogope, kwa kuwa ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote. Maana leo, huko Bethlehemu Mwokozi amezaliwa ndiye Kristo, Bwana. Mtoto amevikwa nguo za kitoto na amelazwa katika hori ya kulia ng’ombe.” *Waulize watoto wataje majina mengine ambayo Yesu aliitwa yaani Kristo, Bwana na Mwokozi. Zingatia ukweli kwamba Yesu aliitwa Mwokozi kwa sababu alikusudiwa kuokoa ulimwengu kutoka katika dhambi zao. Waelezee watoto kwamba Yesu alipokua, alikufa msalabani na kuchukua adhabu ya dhambi zetu ili aweze kuwa Mwokozi wetu. Eleza kwamba neno "Kristo" lina maana kuwa Yeye ni mteule wa Mungu, na neno "Bwana" lina maana kuwa Yeye ni Mkuu.* ***(Luka 2:9-12)***<br>• Ghafla, jeshi kubwa la malaika likajaza anga, na kumwimbia Mungu sifa likisema, “Atukuzwe Mungu juu Mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliopendezwa nao! *Wakumbushe watoto kwamba Mungu kumtuma Yesu duniani awe Mwokozi wetu lilikuwa jambo la kushangaza sana na kwamba, kama vile malaika walivyomsifu Mungu, tunapaswa kumsifu na kumshukuru pia kwa yale ambayo ametufanyia.* ***(Luka 2:13-14)***<br>• Malaika walipoondoka, wachungaji walisemezana wao kwa wao na kusema, “Twendeni Bethlehemu tukaone jambo hili ambalo Mungu ametuambia.” ***(Luka 2:15)***<br>• *Wasaidie watoto kuelewa kwamba Yesu alikuwa zawadi kuu ya Krismasi ambayo Mungu angeweza kutupa sisi sote.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Mungu amtuma Yesu, Mwokozi. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari Muhimu – ***Luka 2:11*** |
| **KUMBUKA** | Waagize watoto wachore picha ya shamba ambapo wachungaji walikuwepo. Tumia vifaa tofauti - pamba, karatasi ya fedha, kadi, kitambaa, pamba, rangi, nk.<br><br>Au waambie watoto wajibu maswali yafuatayo kama njia ya kurejelea habari:<br>• Nani walikuwa kondeni?<br>• Kwa nini wachungaji walikuwa kondeni usiku?<br>• Nini kilitokea angani?<br>• Wachungaji walijisikiaje?<br>• Malaika alisema nani alikuwa amezaliwa?<br>• Ni nini kilijaza anga?<br>• Waliimba nini?<br>• Wachungaji waliamua kufanya nini? |

## C12 Habari ya Tatu

**Wachungaji wamuona Yesu – Habari hii inahusu wageni wa kwanza wa Mtoto.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Wachungaji waliitikia ujumbe wa malaika.<br>• Tunahitaji kuitikia habari njema kuhusu Yesu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 2: 20***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Luka 2: 16-20*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza na watoto waseme kuhusu wakati ambapo walisikia habari njema. Toa mifano ya kibinafsi k.m. kusikia kuhusu kuzaliwa kwa mtoto mchanga au kusikia kuhusu mtu anayekuja kumtembelea mtoto. Waulize walijisikiaje waliposikia habari hizo na kama waliwaambia watu wengine kuhusu habari hizo. Kumbusha habari njema ambayo wachungaji walisikia. (habari ya 2) |
| **FUNDISHA** | • Wakati wachungaji waliposikia habari njema kuhusu Yesu, hawakuweza kusubiri kwenda kujionea Mtoto. Walienda haraka na kumkuta Mariamu, Yusufu na mtoto mchanga. *Walikuwaje na uhakika kwamba wamefika mahali sahihi? (Kidokezo—ujumbe wa malaika) Thibitisha kwamba mtoto alikuwa amelala kwenye hori ya kulia ng'ombe kama walivyokuwa wameambiwa.* ***(Luka 2:16)***<br>• Walipomwona Yesu, hawakuweza kunyamaza bila kusema habari hiyo njema. Walimwambia kila mtu waliyekutana naye juu ya kile kilichotokea. Watu waliowaambia walishangaa na kustaajabia mambo waliyosikia. *Wakumbushe watoto kwamba ukweli kwamba Yesu alizaliwa bado ni habari ya kushangaza leo. Leo, tunajua ukweli wa ajabu kwamba Yesu pia alikufa na kufufuka tena. Kama wachungaji walivyotaka kuwaambia watu waliokutana nao kuhusu Yesu, hata sisi tunaweza kuwaambia marafiki zetu kuhusu habari njema ya Yesu.* ***(Luka 2:17-18)***<br>• Mariamu alikumbuka mambo yote yaliyotukia, na alifikiri sana kuhusu mambo hayo. Wachungaji walirudi kondeni, lakini hawakusahau kamwe mambo ambayo walikuwa wamesikia. Waliendelea kumtukuza Mungu na kumsifu kwa mambo yote makuu waliyoyaona. ***(Luka 2:19-20)***<br>• *Waelezee watoto kwamba wachungaji walipokutana na Yesu, maisha yao yalibadilika, na hawakusahau kamwe mambo yaliyotokea. Tunapomjua Yesu kama Mwokozi wetu, anaweza kubadilisha maisha yetu pia. Kama vile wachungaji walivyomsifu Mungu, tunapaswa pia kumshukuru Mungu kwa kumtoa Yesu awe Mwokozi wetu!*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Wachungaji wamuona Yesu. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari Muhimu – ***Luka 2:20*** |
| **KUMBUKA** | Waambie watoto wajibu maswali yafuatayo kama njia ya kurejelea habari:<br>• Ni nani alikuwa amewaambia wachungaji habari za mtoto mchanga?<br>• Walifanya nini waliposikia habari njema?<br>• Wachungaji walimuona nani walipofika Bethlehemu?<br>• Mtoto Yesu alikuwa amelala wapi?<br>• Wachungaji walimweleza nani kuhusu mambo waliyoona?<br>• Ni nani alikumbuka mambo yaliyotukia na kuendelea kuyafikiria?<br>• Wachungaji walienda wapi baada ya kuondoka Bethlehemu?<br>• Walimsifu nani? |

**<u>C12 Habari ya Nne</u>**

**Yohana ambatiza Yesu – Habari hii inahusu Yesu katika Mto Yordani.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu alibatizwa na Yohana ili kuonyesha kuwa amekuja kuwa mmoja wetu.<br>• Yesu ni tofauti na sisi kwa sababu hana dhambi.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Marko 1: 7***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Marko 1: 1-9*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Waulize watoto kama wamewahi kuona mtu yeyote muhimu akija kuwatembelea nyumbani kwao au shuleni kwao au mjini kwao. Kama hawajawahi, unaweza kutoa mfano wa kufikirika wa mtu muhimu anapowatembelea. Jadili matayarisho ambayo yangefanywa kwa ajili ya mtu huyo anayekuja. Waambie watoto kwamba habari ya leo ni kuhusu mtu aliyeandaa njia kwa ajili ya Yesu. |
| **FUNDISHA** | • Baada ya Yesu kuzaliwa, Biblia haituambii mengi kuhusu maisha yake hadi alipokuwa na umri wa miaka 30. Pengine alikulia Nazareti pamoja na familia yake na aliweza kufanya kazi ya useremala kama Yusufu alivyofanya.<br>• Yesu alikuwa na uhusiano na Yohana. Mara nyingi tunamwita Yohana Mbatizaji. Yohana alikuwa akiishi jangwani ambako alivaa ngozi za ngamia, na chakula chake kilikuwa nzige na asali ya mwitu. ***(Marko 1:6)*** *Zungumzia jinsi jambo hilo lilivyokuwa la ajabu.*<br>• Yohana Mbatizaji alikuwa mhubiri. Kazi yake maalum ilikuwa kuwaandaa watu kwa ajili ya kuja kwa Kristo, Bwana. Watu wengi walikuja kusikiliza ujumbe ambao Yohana alikuwa akihubiri. Watu walipoacha dhambi zao (walipotubu) Yohana aliwabatiza. Maana yake aliwazamisha kwenye maji. *Eleza kwamba sio maji yaliyoosha dhambi zao, bali ilikuwa ni ishara ya kile kilichotokea katika maisha yao.* Aliwaambia kwamba anakuja mtu bora zaidi na mwenye nguvu zaidi kuliko yeye. Alipozungumza kuhusu Yesu alisema, “Mimi sistahili kuvivua viatu vyake”. *Eleza kwamba mtumwa angefanya hivyo kwa bwana wake. Lakini Yesu alikuwa mkuu zaidi kuliko Yohana, kiasi kwamba Yohana hakujisikia kwamba anastahili hata kuwa mtumwa wa Yesu.* Pia alisema siku moja Yesu ataleta Roho Mtakatifu kwa watu. ***(Marko 1:4-5, 7-8)***<br>• Yesu alipokuwa na umri wa miaka 30 hivi, wakati ulifika wa kuanza kuwaita watu kwa Mungu na kuhubiri habari njema ambayo malaika alikuwa amesema siku aliyozaliwa. Yesu aliendа hadi mto Yordani ambako Yohana alikuwa akihubiri na kubatiza watu. Yohana alimbatiza Yesu katika mto Yordani. ***(Marko 1:9)***<br>• *Waelezee watoto kwamba Yesu hakuhitaji kubatizwa kwa sababu ya dhambi yake. Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, kwa hiyo alikuwa mkamilifu na hakuwahi kufanya lolote baya. Yesu alipobatizwa, alikuwa anasogea karibu na watu wenye dhambi ambao ni sisi. Yesu aliamua kuwa kama sisi, wakati hakuwa na dhambi, ili siku moja aende msalabani na kufa kwa ajili ya msamaha wa dhambi zetu.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Yohana ambatiza Yesu. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari Muhimu – ***Marko 1:7*** |
| **KUMBUKA** | Waambie watoto wajibu maswali yafuatayo kama njia ya kurejelea habari:<br>• Yesu alikulia wapi?<br>• Nani alikuwa na uhusiano na Yesu?<br>• Yohana alikula nini nyikani?<br>• Yohana Mbatizaji alisema anakuja nani?<br>• Yohana Mbatizaji alisema kwamba Yesu alikuwa _________ zaidi kuliko yeye. (Jaza neno linalokosekana)<br>• Yesu alikuwa na umri gani alipokuja kumwona Yohana?<br>• Yohana alimfanyia nini Yesu?<br>• Kwa nini Yesu hakuhitaji kusamehewa dhambi Zake? |

# Maelekezo ya waalimu wanaposahihisha masomo

**MASOMO YA DARAJA LA KWANZA:**
- Kurasa nne kwenye kijitabu kina sehemu za kupaka rangi, kujaza maneno machache au kufanya kazi rahisi kila wiki.
- Alama 20 zimewekwa kwa kila wiki na alama 80 kwa kila mwezi.
- Watoto wanaotumia masomo ya Daraja la kwanza hawatarajiwi kuwa wanajua kusoma vizuri. Hivyo basi, tunatarajia wazazi/ walezi/ viongozi wa madarasa kuwasaidia.

**MASOMO YA DARAJA LA PILI:**
- Kurasa 4 kila wiki kwenye vijitabu.
- Habari ya Biblia ipo kwenye somo. Watoto/ wanafunzi wanapaswa kupata baadhi ya maneno kwenye somo, kupaka rangi, kukamilisha Mstari Muhimu na kadhalika.
- Alama 20 zimewekwa kwa kila wiki na alama 80 kila mwezi masomo yanapokamilishwa kwa usahihi.

**KUSAHIHISHA MASOMO YA WAKATI NA BIBLIA**

**VITU VYA KUTUSAIDIA TUNAPOSAHIHISHA**
Waalimu wanaombwa kwanza:
- Kuangalia kila somo na kusahihisha ipasavyo.
- Toa alama kama ulivyoelekezwa.
- Kila mara, tumia wino wa rangi tofauti kusahihisha na kuweka ALAMA YA VEMA (✔) kwenye jibu sahihi.
- Weka au andika jibu sahihi panapostahili na rekebisha makosa yoyote ya maandishi (spelling errors), lakini hakuna alama zinazoondolewa kwa ajili ya kosa hili.
- Toa alama nusu kwa kila jibu ambalo sio sahihi kabisa.
- Jumlisha alama za mwezi na uziandike kwenye nafasi uliyopewa kwa ajili hiyo.

Ni muhimu kuwa mkarimu kama uwezavyo ili kuwatia moyo watoto/ wanafunzi wafanye masomo ya Biblia. Kila mwezi, ni muhimu kwa mwalimu kuandika maneno ya kutia moyo kwenye nafasi iliyowekwa kwa kila mtoto anayemfundisha. Unaweza kuandika kuhusu kupaka rangi vizuri, kufanya kazi safi, alama alizopata mtoto, uelewa wa masomo wa mtoto na kadhalika.

Tunajaribu kutoa mawazo tofauti kama iwezekanavyo. Maswali, maoni, maneno ya kutia moyo na kadhalika, yote yanaweza kutumiwa kuleta utofauti. Kama maoni au usemi mmoja unatumika kila mwezi, watoto watauona hauna maana tena.

**DARAJA LA KWANZA**
**Maoni ya jumla**
“Neema – Ninafurahi kuwa umeanza masomo haya na natumai unayafurahia. Nimependa sana ulivyopaka rangi.
“Je, huwa unaenda shule? Niambie kuhusu shule yako. Ninatarajia kusikia kutoka kwako siku za karibuni.”
“Hongera sana Pendo! Umepaka rangi kwa ustadi kweli! Je, ilikuwa vigumu kupaka rangi ndani ya picha tu? Ulikosea kidogo ulipokuwa unapaka rangi kwenye baadhi ya sehemu za somo la mwisho.”

**Maoni ya Kiroho**
“Umefanya vyema sana Faraja! Jairo alikuwa na furaha kubwa Yesu alipomsaidia.”
“Jibu zuri sana! Habari ya kifo cha Yesu inahuzunisha lakini cha kufurahisha ni kwamba, alifufuka tena.”

**DARAJA LA PILI**
**Maoni ya jumla**
“Jibu zuri sana Wema!– “Ninauhakika kuwa, walimu wako wanafurahia sana kazi zako huko shuleni!”
“Debora, naona kuwa tutasherehekea siku yako ya kuzaliwa hivi karibuni. Je, una maandalizi yoyote ya siku hiyo? Je, ni maadalizi gani? Uwe na siku njema!”
“Umejitahidi kweli. Lakini kuna makosa madogo. Usisahau kuhakiki majibu yako kila mara. Mtoto mzuri!”

**Maoni ya Kiroho**
“Napenda ulivyompaka rangi Mtoto Yesu akiwa horini. Je, si inapendeza sana Mungu kumtuma Yesu ulimwenguni kwa ajili yetu?”
“Napenda sana rangi ulizozitumia! Ilimbidi Zakaria kulipa gharama ya kutoamini maneno ya Mungu. Hakukosa kuamini maneno ya Mungu tena.”
“Majibu mwafaka kweli! Mtu aliyekutana na Filipo kule jangwani alienda akiwa na furaha kweli. Alisikia na kuamini Habari Njema za Yesu.”

## Kiambatisho A – Daraja la Sifuri & la Kwanza Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| C7 | Daudi | **Daudi na Yonathani/ Daudi akimbia asiuawe** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-david-saul/ |
| | | **Daudi Mfalme/Daudi aokoa maisha ya Sauli** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-david-cave/ |
| | | **Daudi awa mfalme** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/fn-david-mephibosheth/ |
| | | **Daudi na Mefiboshethi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-mephibosheth/ |
| | | |
| C8 | Yoshua | **Yoshua awa kiongozi mpya** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-joshua-commander/ |
| | | **Yoshua na nchi mpya** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/sb-rahab-spies/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-joshua-commander/ |
| | | **Yoshua na Yordani** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/sb-joshua-jordan/ |
| | | **Yoshua na Yeriko** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-joshua-commander/ |

## Kiambatisho A – Daraja la Pili Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| C7 | Daudi | **Daudi akimbia asiuawe** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/david-jonathan/ |
| | | **Daudi aokoa maisha ya Sauli** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/david-saul-cave/ |
| | | **Daudi awa mfalme** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/saul-last-days/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/david-ark/ |
| | | **Danieli – Katika tundu la simba** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-daniel/ |
| | | |
| C8 | Yoshua | **Yoshua awa kiongozi mpya** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-joshua/ |
| | | **Yoshua na nchi mpya** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-joshua-commander/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joshua-rahab-spies/ |
| | | **Yoshua na Yordani** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joshua-jordan/ |
| | | **Yoshua na Yeriko** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joshua-jericho/ |

## Kiambatisho B – Daraja la Sifuri & la Kwanza Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| C9 | Eliya | **Eliya amtii Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/sb-elijah-food/ |
| | | **Eliya amtumaini Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/sb-elijah-food/ |
| | | **Eliya amtumikia Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-prophet-elijah/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/rg-elijah-baal/ |
| | | **Eliya amuomba tena/amsahau Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/rg-elijah-baal/ |
| | | |
| C10 | Elisha | **Elisha, Msaidizi mpya kutoka kwa Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/rg-elijah-elisha/ |
| | | **Elisha amsaidia mjane maskini** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/rg-elisha-oil/ |
| | | **Mungu amtumia Elisha kuponya mgonjwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/rg-elisha-naaman-1/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/rg-elisha-naaman-2/ |
| | | **Elisha na mtumishi wake mwenye tamaa ya mali** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/rg-elisha-naaman-2/ |

## Kiambatisho B – Daraja la Pili Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| C9 | Eliya | **Eliya amtii Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/sb-elijah-food/ |
| | | **Eliya amtumaini Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/sb-elijah-food/ |
| | | **Eliya amtumikia Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-prophet-elijah/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/elijah-prophets-baal/ |
| | | **Eliya amsahau Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/elijah-horeb/ |
| | | |
| C10 | Elisha | **Elisha – Wito wa kufuata** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/elijah-elisha/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/elijah-chariot/ |
| | | **Elisha – Faraja kwa ajili ya rafiki** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/elisha-boy/ |
| | | **Elisha – Kutakasa mwenye ukoma** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/elisha-naaman/ |
| | | **Elisha – Kudanganya kwaadhibiwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/elisha-naaman/ |

## Kiambatisho C – Daraja la Sifuri & la Kwanza Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| C11 | Yona | **Yona ndani ya merikebu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jonah-preschool/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/bpa-jonah/ |
| | | **Yona baharini** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jonah-preschool/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/mk-jonah/ |
| | | **Yona ahubiri Ninawi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/bpa-jonah/ |
| | | **Yona amwomba Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/mk-jonah/ |
| | | |
| C12 | Habari ya Krismasi | **Mungu amtuma Mwanae, Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/birth-jesus-preschool/ |
| | | **Mungu amtuma Yesu, Mwokozi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-christmas-story/ |
| | | **Wachungaji wamuona Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-christmas-story/ |
| | | **Yohana ambatiza Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-jesus-baptised/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/mk-john-baptist/ |

## Kiambatisho C – Daraja la Pili Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| C11 | Yona | **Yona ndani ya merikebu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/mk-jonah/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/bpa-jonah/ |
| | | **Yona baharini** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/bpa-jonah/ |
| | | **Yona ahubiri Ninawi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/mk-jonah/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/bpa-jonah/ |
| | | **Yona amwomba Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/mk-jonah/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jonah-disobeys/ |
| | | |
| C12 | Habari ya Krismasi | **Mungu amtuma Mwanae, Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ed-jesus-birth/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/bpa-christmas/ |
| | | **Mungu amtuma Yesu, Mwokozi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/christmas-shepherds/ |
| | | **Wachungaji wamwona Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/christmas-shepherds/ |
| | | **Yohana ambatiza Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/lgr-john-baptist/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/wdv-john-baptist/ |

© Bible Educational Services 2020
(FBI links 2023)

www.besweb.com

Registered Charity UK CIO 1186004

Swahili - 04/2024